


NI MIMI, MSIOGOPE

 Habari za jioni, marafiki. Hakika, sistahili pongezi kubwa kama nilizopewa hivi punde na Ndugu Bigby, Natumaini ningeweza kuishi kufikia kitu kama hicho. Nami nina furaha, usiku wa leo, kurudi hapa. Tumeninii tu, tukipitia nchini, nasi tulikuwa pamoja na nanii, Ndugu Parker Thomas katika mkutano wake, na nilipojua ya kwamba tungekuwa katika wilaya hii, daima nilikuwa na upendo mwingi na heshima kwa Ndugu Bigby, na kwa watu hawa, niliyahesabu kuwa ni majaliwa makuu kuja usiku wa leo, na kwa ajili ya usiku wa leo na kesho usiku.

² Na kujua, basi, pia, ninasikia tu kwamba Ndugu Ned Iverson, rafiki msiri, mhudumu mashuhuri wa Injili, ataendelea. Nami nilifikiri ningekuwa usiku wa leo, nami nilihubiri sana huko juu, mara ya mwisho katika mkutano huo, mimi, karibu nilihubiri mapafu yangu yaishie kwa mahubiri, naye Ndugu Ned atahubiri hapa chini, na kwa hiyo nilifikiri ningekuwa tu na kuzungumza nanyi kuhusu Yesu, yale tu niliyojua kumhusu, na kuwaombea wagoonjwa.

³ Na kwa hiyo, kama ninavyokumbuka, wakati kanisa hapa lilipokuwa, ninaamini lilipokuwa ndio kwanza lijengwe, ama, Ndugu Bigby alikuwa ndio kwanza tu alichukue, ama kwa njia fulani, nami kamwe sitasahau siku hizo tukufu ambazo tulikuwa hapa. Nilikuwa nikizungumza, nikishuka barabarani, Ninaamini imekuwa yapata—yapata miaka sita na miezi mitatu, ama kitu kama hicho, tangu nilipokuwa hapa. Na watu hawa wazuri kote kote kusini na mashariki, ni majaliwa makubwa sana kufanya ushirika.

⁴ Sasa, usiku wa leo, tunaye mchungaji wetu kutoka maskanini, ambaye—ambaye huchukua mahali pangu wakati nimeondoka, nadhani labda ametambulishwa, Ndugu Neville. Pia tunao wachungaji wengine hapa wa makanisa shirika, Ndugu Bryant, nadhani wote, Ndugu Collins. Ndugu Willard Collins, mhudumu wa Kimethodisti, ndio kwanza ampokee Roho Mtakatifu hivi majuzi, naye yuko katika imani, na Ndugu Neville pia alikuwa mhudumu wa Kimethodisti, Ndugu Jackson alikuwa mhudumu wa Kimethodisti, na kwa hiyo inaonekana kana kwamba Wamethodisti walio njiani mwetu wanakuja moja kwa moja. Kwa hiyo—kwa hiyo hapo . . .

⁵ Mwajua, ninapenda kuwazia hili kama kile kisima cha mwisho ambacho Yakobo alichimba, “Kuna nafasi kwa ajili yetu sote,” mwajua, hakuna mtu anayepaswa kutufukuza. Na kuwazia hivi majuzi usiku, ya kwamba Pentekoste kweli si—

si, dhehebu, ni—ni—ni ushirika, Ni tukio, nasi sote tunaweza kushirikiana huku na kuwa na wakati mzuri sana.

⁶ Na kwa hiyo, kuwa hapa usiku wa leo, na kujaribu kutoshea mimbara ambapo mwalimu mwema kama Ndugu Bigby, hilo ni agizo kubwa, nami nisingejaribu kulifanya hata kidogo. Na halafu nikijua ya kwamba baada ya mimi—mimi kuondoka kesho, ama, kesho usiku, kwamba Ndugu Ned Iverson. . .

⁷ Nina hakika nyote mnamjua Ndugu Ned, na Ndugu Vayle, na hao walimu mashuhuri *kule*, na baba ya Ndugu Ned, mtu mashuhuri, mmoja wao, hudumani siku hizi. Na—na jamaa mdogo kama mimi, ambaye karibu sijui ninii yangu. . . Ninajua tu ABC zangu, hizo ni karibu zote. Mnajua hiyo ni nini? “Kumwamini Kristo Daima,” *ABC*. [Kiingereza: Always Believe Christ—Mfa.] Hiyo ni kweli. Kwa hiyo mimi, hizo ni karibu yote nijuayo, nadhani ingenibidi kujua. Hao wengine hapa wanajua, inawabidi ninyi nyote kuijaza hapo, mwajua, ili tu kuingia. Kwa hiyo hilo ni sawa kabisa.

⁸ Sisi ni. . . Laiti ningaliweza kukaa juma hili na kumsikiliza Ndugu Ned, na kuwa na ushirika mwingi sana pamoja nanyi watu na mchungaji mzuri, lakini sina budi kwenda nyumbani Alhamisi. . . Jumatano asubuhi. Nafika huko wakati fulani Alhamisi usiku, saa tatu, saa nne. Saa kumi ama kumi na moja Alhamisi asubuhi sina budi kuondoka kwenda Cow Palace huko Pwani ya Magharibi, na kuwa Los Angeles kuanzia huko siku chache tu kabla, ama, baada ya mimi kuondoka hapa.

⁹ Kisha nipande Pwani ya Magharibi, kote mpaka huko Washington, Oregon, na huko Canada, na labda Anchorage, Alaska, kufunga ibada. Kisha nirudi na kwenda ng’ambo huko—huko Tanganyika, Uganda, Kenya, na Afrika Kusini, na huko chini kupitia huko, bila shaka ninahitaji maombi yenu.

¹⁰ Nadhani mnashangaa ni kwa nini nina makovu usoni mwote. Labda wengi wenu mlijua, yapata majuma manne tu yaliyopita bunduki kubwa ya Weatherby Magnum ililipukia usoni mwangu, na yapata, loo, tani sita za presha ziliniipiga moja kwa moja usoni. Ingeyang’oa tu mabega, kichwa, na kadhalika, lakini mwajua, Yeye alijua ilinibidi kuja hapa bado, kwa hiyo aliniacha tu ili niweze. Kwa hiyo Yeye hakunichukua wakati huo.

¹¹ Na kwa hiyo, nilikuwa. . . Daima nilipenda kulenga shabaha na kuvua samaki, nami kwa namna fulani nina furaha Bwana aliniruhusu kufanya hivyo, kwa sababu ninapenda kuwa nje katika maumbile. Mtu fulani alikuwa ndiyo kwanza anipe bunduki, ilikuwa ni bu—bunduki iliyogeuzwa, na kwa hiyo sehemu ya kichwa haikutobolewa ndani yake, nami nikatia risasi ndani yake, nikainuka nilenge shabaha, na hayo tu ndiyo niliyoona, ilikuwa ni moto mwekundu yapata urefu wa *lile* dari. Nao mtutu wa bunduki ukarushwa yadi hamsini mbele yangu, nalo tako na bolti vikarushwa yadi ishirini na tano au thelathini

nyuma yangu, ikakata vichaka na miti na kadhalika karibu nami. Nami sijui, ni Mungu tu aliyenijalia kuishi, ndiyo yote.

¹² Nami nashangaa haikuyang'oa macho yangu. Iirusha vipande kadhaa moja kwa moja kwenye fuvu la kichwa *pale*, na kugonga-. . .vikapitia kwenye midomo hapa, na kugonga jino hilo huko nje, ikango'a kichwa chake. Ndipo vipande kumi na vitano vikaenda chini tu ya jicho, vikafanya nusu mwezi, vikaizuia kuyang'oa macho.

¹³ Walinipeleka kwa daktari fulani, akasema, “Jambo pekee nijualo, kwamba hapana shaka Bwana mwema alikuwa ameketi pale, wala hakuwa tayari kwa mtumishi Wake kuondoka bado.” Ilionekana kana kwamba Shetani hakika alikuwa akijaribu kwa bidii. Lakini mwajua, nina—nina furaha sana kwamba Yeye ndiye Eneo letu la Usalama, Yeye—Yeye ni Mahali ambapo tunaweza kuja na—na kujisikia salama.

¹⁴ Nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku juu ya *Jina La Bwana Ni Ngo—Ngome, Ambapo Wenye Haki Hukimbilia Humo, Nao Wako Salama*. Hivi hamna furaha kuwa humo ndani, usiku wa leo? Eneo kuu la Usalama ambapo, mishale yote ya ibilisi inakingwa na ngao yetu ya imani, kujua ya kwamba tumesimama katika Eneo hilo la Usalama, tumetia nanga katika Kristo, salama tuwezavyo kuwa humo ndani. Si hata mauti, yenyewe, yanaweza kutudhuru, tayari tumekufa. Maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, yametiwa muhuri humo ndani kwa Roho Mtakatifu. Si ni ajabu hiyo?

¹⁵ Nilikuwa nikizungumza, huko mkutanoni hivi majuzi usiku. Nikasema. . .Sininii. . .Mambo ninayosema si mengi sana, lakini mara kwa mara Roho Mtakatifu hunipa Jambo la kusema, nami ninalithamini sana, nalipenda tu. Naye alinipa kitu fulani, wazo fulani hivi majuzi usiku, huko chini nyumbani maskanini kabla ya kuja. Na i—ilionekana tu kuwa kitu *fulani* cha maana sana kilichonishika tu.

¹⁶ Nilikuwa nikiwazia juu ya ushahidi, nami nilikuwa nikiwazia wakati Yoshua aliposhuka, ama, vema, kwanza wakati Israeli, watu wa Mungu wote walipokuwa utumwani, walikuwa watumwa, nao—nao iliwabidi kuchukua walichopewa, wangetupywa mikate iliyoota kuvu, wao. . .hivyo ndivyo ilivyowabidi kuula. Kama walikuwa na bi—binti mzuri, nao Wamisri walitaka kumchukua msichana huyo na kumbaka, ninii yoyote. . . wasingeweza kufanya lolote kulihusu. Walikuwa na mwana, jamaa mzuri, kama walitaka kumwua, hakuna kitu wangeweza kufanya, walikuwa watumwa. Ni maisha ya jinsi gani hayo yalikuwa kwa watu wa Mungu, kulazimika kuishi katika hali kama hiyo!

¹⁷ Lakini siku moja, kutoka nyikani, akaja nabii huku Nguzo ya Moto ikimfuata. Naye akawaambia ya kwamba kulikuwako na nchi iliyojaa maziwa na asali, nao wangeweza kuwa na makazi

yao wenyewe, wawalee watoto wao, na kuishi kwa amani, Mungu aliwapenda, alikuwa anaenda kuwapeleka kwenye nchi hiyo. Hakuna hata mmoja wao aliyewahi kuwa kule, mwajua, i—iliwabidi tu kuamini alilosema, kwa hiyo wakamfuata huko nje.

¹⁸ Wakafika mahali paitwapo Kadeshi-barnea, ambapo tunafahamu kuwa ndicho kiti kikuu cha hukumu. Nayo inadhaniwa kuwa ni oasisi huko jangwani, ambako kuna kisima kikubwa, na chemchemi ndogondogo, ambazo tungeweza kuzielezea kwa mifano, na kusema kwamba ni Kiti cha Enzi cha Mungu, na vile viti vidogo vya hukumu, makanisa, milango ya kutokea, ambapo hukumu huanzia nyumbani mwa Mungu.

¹⁹ Lakini hata hivyo, miongoni mwa hilo kundi hapo kulikuwako na shujaa mkuu miongoni mwao, jina lake lilikuwa Yoshua, ambalo linamaanisha “Yehova-Mwokozi.” Naye Yoshua akalitangulia lile kundi, akaenda, akavuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, naye akaleta ushahidi kwamba hiyo nchi ilikuwako, nayo matunda yalikuwa ya kupendeza. Watu wawili walibeba kichala cha zabibu, wangeweza kuonja lile tunda kabla hata hawajafika kule, wakijua ya kwamba lilikuwa ni ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri, Mungu hakuwa amewadanganya, nabii hakuwa amewadanganya, nchi ilikuwako, nao walikuwa moja kwa moja mpakani mwake.

²⁰ Wakavuka wakaingia humo nchini, wakapewa sehemu mbalimbali, makabila yao. Ndipo wakalea familia za—zao, wakapanda mazao yao. Wakaishi kwa amani, walikuwa ni taifa, walikuwa watu. Lakini hatimaye, uzee ukawapata, nao wakafa, ardhi hiyo ndogo ikajaa madoadoa ya makaburi kando ya vilima. Kwa macho yaliyojaa machozi wakatembea juu ya kaburi la aliyekuwa mtakatifu kuliko wote, walipokuwa wakiwazika wapendwa wao.

²¹ Ndipo siku moja, akaja Shujaa mwingine mkuu, alikuwa Shujaa wa hao wote, Yehova aliyedhihirishwa katika mwili, Yesu Kristo, Mwanawe. Akashuka, Naye akawaambia ya kwamba kulikuwa na Nchi iliyo mbali mno na nchi hii, kulikuwa na Nchi ambamo watu hawakufa tena. Naye akasema, “Kuna Uzima baada ya mauti.” Naye akafundisha hayo kwa muda wa miaka mitatu na nusu.

²² Ndipo siku moja akaja Kadeshi-barnea, ambako alistahimili hukumu kwa ajili yetu sote, kiti cha hukumu cha Mungu, ambapo Mungu alimiminia uovu juu Yake, na adhabu ya uovu wetu, ghadhabu ya Mungu juu Yake. Naye akabeba katika mwili Wake dhambi zetu, kisha akavuka mto tunaouita, “Yordani,” mauti.

²³ Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, kama Yoshua, Yeye akarudi pamoja na ushahidi, mwanadamu huishi tena baada ya mauti. Walidhani ilikuwa ni roho, Yeye akasema, “Niguseni Mimi, roho haina mwili na mifupa kama niliyo nayo.” Kasema,

“Mna chakula?” Wakampa samaki na mkate, Naye akala. Ndipo akasema, “Nitawapa Arabuni ya Nchi hii. Lakini ngojeni huko juu Yerusalemu mpaka mtakapopata Malipo ya Kwanza.”

²⁴ Kwa hiyo wakapanda kule juu na kungojea, ndipo Arabuni ikarudishwa ya Nchi hiyo, na leo hii tunaweza kuifurahia Hiyo. Sisi sasa, tunajihesabu kuwa tumekufa na kuzikwa pamoja Naye katika ubatizo, tumefufuliwa pamoja Naye. Tukinena kiroho, sisi sasa, usiku wa leo, tumeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tumefufuka pamoja Naye.

²⁵ Sasa tuko katika Mwili wa Kristo, Wakorintho wa Kwanza 12, “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Kwa kitu gani? Hiyo ndiyo Arabuni ya urithi wetu. Tayari tuna Malipo ya Kwanza juu yake, kwamba tunajua tulipita kutoka mautini kuingia Uzimani. Tunaangalia nyuma na kuona mahali tulipokuwa wakati mmoja na mahali tulipo sasa, kuna dhambi ulimwenguni huko chini, nasi tuliinuliwa juu yake, tukiketi pamoja Naye, Mfalme wetu, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Ni Ushahidi wa jinsi gani!

²⁶ Wala hata mauti yenyewe... Wakati shujaa mashuhuri, Paulo, alipokuja kukabiliana nayo, alipaza sauti, “Ee mauti, u wapi mwiba wako? Au, kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Afadhali niache hayo, ningekuwa nikihubiri.

²⁷ Nilikuwa kwenye mkutano mkuu si muda mrefu uliopita nami nikamsikia mama mweusi akitoa ushuhuda. Inasikika fidhuli, samahani, tafadhali, kwa ujuvu wake, lakini inaonekana inafaa sasa hivi. Alisimama kutoa ushuhuda, anasema, na kama kuna watu weusi wowote karibu, simaanishi kutoa usemi huu kijeuri, anasema, “Fema, mimi taka kumshukuru Bwana,” akasema, “Mimi...kwa kuwa hapa.” Akasema, “Na—najua ya kwamba siiko vile ninavyopaswa kuwa,” kisha akasema, “halafu ninajua tena, siko vile ninavyotaka kuwa, lakini,” akasema, “jambo moja nijualo, siiko vile mimi nilivyokuwa.” Kwa hiyo, nafikiri hiyo ni kweli.

²⁸ Hilo ni jambo moja tunaloweza kujua kwa Ushahidi huu, hatuko jinsi tulivyokuwa, hiyo *pale huko* chini, chini yetu. Nasi tumefufuka katika Kristo, tumeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu pamoja na Ushahidi wa Uzima wa Milele, kwa kumpokea Roho Mtakatifu, kama alivyoahidi kwenye Siku ya Pentekoste tungempokea.

²⁹ Nami niko hapa, usiku wa leo, kushiriki jambo hilo pamoja nanyi. Nami...Ndugu Iverson, kama nilivyosema, atakuwa akihubiri. Nafikiri wana ibada kesho hapa, nami ningesema, njoni mkamsikie mtumishi huyu mashuhuri wa Kristo, mvulana wa thamani. Ndugu Iverson anajitahidi, nasi tumeketi pamoja, nami ninajua Mungu ana jambo la kumfanyia Ndugu Iverson.

30 Yeye anazungukazunguka tu, akijaribu kupata njia yake, kama nilivyokuwa nikieleza hivi majuzi usiku, yule mwanamke akijaribu kugusa vazi Lake. Kila alipojaribu kugusa, mbona, mtu fulani angemzuia, lakini aling'ang'ania, alikaa tu pale mpaka akapata ule mguso. Na hiyo ndiyo njia, endelea tu kusukuma mpaka utakapopata ule mguso, hiyo ndiyo njia pekee ya kufanya hivyo; ng'ang'ania.

31 Basi sasa, nimekuja kuwaombea wagonjwa, wakati Ndugu Iverson akija kuwahubiria watakatifu, na kadhalika. Na sasa, ningependa kusema jambo hili kabla tu hatujasoma somo, nami sitawaweka kwa muda mrefu sana, kwa sababu ya . . . Huko juu niliaweka watu mpaka karibu usiku wa manane kila usiku. Na ndiyo kwanza nimalizie kuhubiri nyumbani, mahubiri mafupi tu, saa sita, wala sijisikii vizuri *hivyo* usiku wa leo, hata hivyo.

32 Kwa hiyo mimi, kwa hiyo sasa, nafikiri, hata hivyo, wakati tukiwa . . . Tunataka kuja kwenye ushirika sasa kwa yapata dakika thelathini kwenye Neno, kidogo tu, kwenye Neno la mchezo wa kuigiza.

33 Nami nafikiri kwamba moja ya mambo makuu sana ambayo Mkristo yeyote angeweza kuwazia, ingekuwa ni kujua ya kwamba wao, sasa, wako katika Uwepo wa Yesu Kristo. Tunazungumza juu Yake, tunamwabudu, tunawaza juu Yake, na tunasoma habari Zake, na sasa, kuwa na ushahidi wa moja kwa moja ya kwamba Yeye aliyeliandika Neno yupo hapa pamoja nasi. Tunamwona Yeye akitenda kazi, Uwepo Wake, kama tu kuona kitu Fulani kikisogea kwenye kusanyiko, na pamoja na watu, na ndani ya watu, na juu ya watu, na kupitia kwa watu: Mungu pamoja nasi, ndani yetu, kupitia kwetu, juu yetu. Nafikiri ni faraja ya ajabu, sivyo?

34 Na sasa, nivumilieni kwa dakika chache tu, ninaposoma Maandiko fulani. Kama mngetaka kuyageukia, ningetaka kufungua Mathayo mlango wa 14 na kusoma se—sehemu, yapata kifungu cha 22 mpaka yapata kifungu cha 27. Na labda kutokana na hili Mungu ataturuhusu kutoa muktadha mdogo.

Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipokwisha kuaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba: na ilipokuwa jioni, alikuwa huko peke yake.

Na kile chombo kilikuwa kimefika katikati ya bahari, kinatabika sana na mawimbi, maana upepo ulikuwa wa mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari.

Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga mayowe kwa hofu.

Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.

35 Napenda kutumia hayo kama somo: *Ni Mimi, MsioCOPE.*

36 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Wakati tumeinamisha vichwa vyetu na ninatumaini ya kwamba moyo yetu imeinamishwa, pia, katika Uwepo Wake, kama kungekuwako na haja miongoni mwa watu kwa ajili ya jambo *fulani* kutoka kwa Kristo, nawe ungetaka nikukumbuke, naomba uinue tu mikono yako, naye Mungu atajua kilicho chini ya mkono wako. Asanteni.

37 Mungu aliye mwingi wa Neema, aliyemfufua Bwana Yesu katika wafu, na amemweka miongoni mwetu sasa kwa miaka hii elfu mbili, na siku moja atauwasilisha mwili huo mtukufu ukija duniani mara ya pili kulichua Kanisa Lake, tuna furaha sana kwamba pumzi hiyo kuu ya tumaini inatulia ndani ya nafsi zetu, usiku wa leo.

38 Tuna furaha, Bwana, kwa sababu hatuko peke yetu, usiku wa leo, katika ushirika huu wa furaha hii kuu, kuna maelfu mengi kote ulimwenguni ambao wanashiriki majaliwa haya, tunapodai ya kwamba sisi si wa ulimwengu huu, bali sisi ni wasafiri na wageni, tunapitia tu hapa. Hatuuajali ulimwengu, kusudi letu pekee ni kuufanya ulimwengu umwone Yeye Yule aliyekufa kwa ajili yao.

39 Na kwa watoto wagonjwa wa dunia hii, wana majaliwa ya kuja kwenye Chemchemi hii kuu, na mle ndani wanajua ya kwamba ugonjwa wao umelipiwa, Yesu wa Nazareti, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

40 Nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili, kujua ya kwamba tuna mlango huu mzuri sana wa kutokea, usiku wa leo, kwa ninii zetu zote, kuondolea mbali wasiwasi wetu wote, shida zetu zote, maradhi yetu, magonjwa, na hata hofu yenyewe ya mauti, nayo mauti yatatukimbia tunapomkiri Yeye, na kumwamini Yeye.

41 Tumefundishwa, kwa Maneno Yake Mwenyewe, katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Mungu, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hilo! Hayo ni Maneno ya Mungu wa Milele, nasi tunayathamini *sana* moyoni mwetu, tukijua ya kwamba Mbingu na nchi pia zitapita, bali Neno hilo halitashindwa kamwe. Kote katikati ya shida, majaribu, mabomu ya atomiki, kupitia kwenye

vivuli vya mauti, linaendelea kuishi moja kwa moja, kwa sababu ni Neno la Mungu.

⁴² Mikono iliinuliwa usiku wa leo, Baba, tuliona karibu asilimia mia moja kwenye jengo hili, hata ndani na nje, roshani na kila mahali, kwamba kulikuwa na mikono iliyoinuliwa, ni wahitaji, Baba, ninakuhitaji, sote tunakuhitaji. Hivi hutakuja, Bwana? Mtembelee kila mmoja wetu, usiku wa leo, utupe shauku ya moyo wetu. Tunatamani kukuona Wewe, na kukupenda. Tunajua Wewe unapendeka sana, umejaa neema na rehema. Basi uturehemu sisi maskini, wahitaji usiku wa leo, kwa kuwa tunakupenda, na kuliitia Jina Lako juu yetu, sisi ni Wakristo. Asante, Baba.

⁴³ Tutakutarajia Wewe ututembelee sasa, ninajua umefanya hivyo katika kuimba, na katika maombi, na kadhalika, nami naomba, Baba, Wewe utaendelea pamoja nasi usiku kucha.

⁴⁴ Kesho, uwe pamoja na Ndugu yangu mpendwa, Ned. Ninaomba ya kwamba Wewe utamtia mafuta, Bwana, pamoja na ibada ya kesho usiku, na ibada zinazoendelea.

⁴⁵ Mungu na ambariki Ndugu yetu Bigby hapa, mwenye neema sana, kanisa hili zuri sana, na kondoo hawa ambao amewachunga, Mungu, kuwa pamoja na mtu huyu mkuu na umwongoze na kumwelekeza, Bwana. Na jalia awalishe wana-kondoo na kondoo wa Mungu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁶ Sasa, hapana shaka ilikuwa karibu wakati wa kutua kwa jua, ilikuwa ni siku ya kutisha sana, presha nyingi ilikuwa imeingia. Na hizo ni siku mbaya, wakati presha imeongezeka. Na popote Yesu alipoenda, daima kulikuwa na msongamano wa umati. Nayo hii ilikuwa ni siku ya kipekee. Ndipo yapata wakati jua lilipoanza kutua, ninaweza tu kuona hiyo misuli mikubwa mikubwa kwenye mgongo huo wenye misuli migumu wa huyo mvuvi, huku yeye, akisukuma mashua ukingoni.

⁴⁷ Naye alikuwa mtu mwenye nguvu, aliyajua hayo maziwa, alikuwa amevua samaki kwayo tangu alipokuwa mvulana mdogo. Baba yake alikuwa mvuvi kabla yake, hiyo ilikuwa ndiyo kazi yake, alijua aina za hayo maji, jinsi ya kuvua samaki, na mahali pa kuvulia. Basi walipokuwa wakiupindua ule mtumbwi mdogo, ndipo Simoni anakuja, labda, katikati ya hiyo mashua, anaketi karibu na ndugu yake, Andrea, na kuchukua kasia.

⁴⁸ Sasa, meli za siku hizo hazikuwa kama zilivyo sasa, wakati huo ziliendeshwa na nguvu za wanadamu, wakati mwingine zilikuwa na matanga juu yao, wakati upepo ulipokuwa mzuri, wangeweza kusafiri, wakati upepo haukuwa ukivuma, wange-wangepiga makasia.

⁴⁹ Na jinsi meli za uvuvi zilivyokuwa [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.), walikuwa na labda seti sita ama nane za makasia. Halafu basi, hayo makasia yalikuwa

makubwa sana, yangehitaji watu wawili, mmoja upande mmoja, mmoja upande mwingine, kwa sababu wakati mawimbi na kadhalika, dhoruba juu ya bahari na maziwa, ingewabidi kuvuta kwa nguvu kuielekeza hiyo mashua ndogo la sivyo ingepinduka, iingie kwenye mawimbi vizuri kabisa.

⁵⁰ Ninyi watu mnajua, mnaoishi kando ya maziwa haya hapa, jinsi inavyokubidi kuielekeza shetri ya mashua ili kuyapembeja mawimbi, yasiye, juu na chini, yangeuvurumisha moja kwa moja chini, yaijaze maji, huna budi kuyapembeja yote. Basi ilihitaji mikono yenye nguvu na watu wenye ujuzi kuivuta hiyo mashua. Karibu wote walioishi karibu na Galilaya walikuwa wavuvi, hiyo ilikuwa nchi kubwa ya uvuvi, nao walitumia muda mwingi kwenye hayo maziwa.

⁵¹ Nao walikuwa na siku kuu, mambo makuu. Na, bila shaka, wakati . . . Kuna jambo fulani kuhusu ushirika unapokutana na mtumishi wa Kristo, unawasalimia kwa mkono, na kama wamewahi kuwasiliana na Yesu, kuna kitu fulani tu kuwahusu hata huwezi kamwe kuwasahau, kuna kitu ambacho—ambacho huvuta, hata u—unachukia tu kuwaona wakiondoka.

⁵² Mara nyingi nimeshangaa jinsi ambavyo Wakristo wangeweza kuzozana wao kwa wao, ama *kutofautiana*, kwa sababu ya tofauti ndogo na kadhalika, wakati wanajua kweli kwamba huyo ni ndugu ama dada anayempenda Bwana.

⁵³ Tulikuwa tukiimba wimbo mdogo maskanini mwetu, miaka mingi iliyopita, na wengi . . . Nadhani bado mnao. Nilikuja tu, nikaja huku kwa gari, ndipo nikasikia huo uimbaji mzuri. Nami . . . Ule wimbo tuliokuwa tukiimba, ni wa zamani:

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama wa huko juu.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumainia kukutana tena.

⁵⁴ Laiti Kanisa lingeweza tu kujisikia hivyo! Kama kila Mkristo angeweza kuhisi huzuni za mwenzake, na mizigo, na kadhalika, si lingekuwa ni jambo la ajabu? Yesu anatutaka tuwe hivyo, Yeye alisema, ombi Lake lilikuwa kwamba tuwe kitu *kimoja*. Ninaamini asingeweza kumwomba Mungu lolote, pasipo Mungu kumjalilia, kama vile Martha alivyosema, “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupaa.”

⁵⁵ Ninaamini kwamba mtu . . . Ninaamini Wakristo wote, hata sasa, wanajisikia hivyo mmoja kwa mwingine. Hiyo ni kweli. Bila shaka, tunajua lile shamba kuu la mavuno, kulikuwako na magugu, na kwekwe; na mfano wa jarife lililotupwa ndani, kulikuwa na ya kila namna, yote hayana budi kuja pamoja.

Lakini ninaamini Mungu anawajua watoto Wake wa thamani ambao wametawanyika kote kule katika ulimwengu huu wenye giza.

⁵⁶ Wakati meli ilipoondoka, hao watu wapendwa wamesimama ukingoni, wakipunga mikono, “Kwaherini. Rudini mkatuone tena. Tulifurahi sana kukutana nanyi. Na sasa tunajua ya kwamba sisi ni raia wenzenu wa Ufalme mkuu wa Mungu, sisi ni sehemu ya familia Yake. Hivi hamtarudi kutuona tena?” wakati hiyo meli ikiingia baharini.

⁵⁷ Nanyi mwajua, labda wangepiga makasia kadhaa kwa nguvu, kisha wainuke na kupunga mkono, na kuipiga mashua tena, nayo hiyo maskini meli kwenye bahari tulivu ikisogea wakati hao wavuvi mashuhuri wakivuta makasia. Na, hapana shaka ilikuwa ni tamasha ya ajabu sana kuiangalia hiyo meli ndogo, ilipoendelea kufifia na kufifia, nalo lile kundi ufukoni likazidi kufifia na kufifia, mpaka hatimaye wakafifia wakati jua lilipoanza kutua; kuvuta mashua ni kazi ngumu. Nitawazia tu, sasa, ya kwamba nimeketi kwenye kiti cha nyuma, nikisimulia jambo lililotukia huko nje.

⁵⁸ Na sasa, ninawaona waliposimama kupumzika kidogo tu, wakivuta makasia yao ndani, na kupangusa jasho usoni mwao. Hapana shaka ilikuwa, nitasema kijana Yohana, baada ya kuketi wakivuta pumzi yao kwa dakika chache, kwa sababu bado walikuwa na masafa mrefu sana ya kwenda, karibu usiku mzima wa kuvuta. Ndipo basi, akivuta pumzi yake, akaangalia kote, na kusema, “Ndugu,” na mkutano huu wa ushuhuda watakaofanya sasa, naye akasema, “hebu na tufanye mkutano wa ushuhuda tunapongojea. Naye atatufikia baada ya kitambo kidogo, basi hebu tufanye mkutano wa ushuhuda.”

⁵⁹ Nami ni—ningetaka kufanya hivyo usiku wa leo, tunapozungumza juu Yake. Hakika, Yeye atatufikia baada ya kitambo kidogo, hapa mahali fulani, basi hebu tuzungumze tu juu Yake kwa muda kidogo. Hebu na tusikie shuhuda walizokuwa nazo.

⁶⁰ Ninaweza kumsikia Yohana akisema, “Ningetaka kushuhudia kwanza,” kwa sababu Yohana alikuwa ni jamaa mdogo. Akasema, “Mnajua, hatuwezi kamwe kushuku tena, kwa kweli hatuwezi kufanya hivyo, kwa sababu ya yale tumeona leo, tunajua ya kwamba haidhuru ni Mafarisayo wangapi, ama ni waandishi wangapi wanaosema kwamba hili ni kosa, sisi tunajua ni kweli. Sisi hatumfuati nabii wa uongo, tunamfuata Kristo wa Bwana.”

⁶¹ Naye akasema . . . Huenda nilisema kitu kama hiki: “Miaka mingi iliyopita, kama mvulana mdogo, nililelewa karibu na—na Yeriko. Nami ninaweza kukumbuka zile siku ambazo ningecheza huko nje kando ya kilima katika majira ya kuchipua. Ningali ninaweza kumwona yule mama yangu mrembo, Myahudi.

Wakati Baba alipokuwa ameenda shambani kufanya kazi, alikuwa akinipembeza nilale alasiri, naye angeketi nje ba—barazani, na kunipembeza nipate kulala, na kunisimulia hadithi za Biblia.

⁶² “Naye angeelekeza chini kwenye kile kivuko, chini tu ya Yeriko, na kusema, ‘Yohana, usisahau, kumbuka, hapo ndipo yule Yoshua mkuu, mwenye nguvu, alipovuka bahari, ama, ninii...katika mwezi wa Aprili, ama—ama, Yordani. Naye Yehova Mkuu akayazuia maji, tukiingia katika nchi ya ahadi. Na moja kwa moja kwenye barabara ile inayotelemka *kule*, yule nabii mkuu Eliya na Elisha walitembea wameshikana mikono, wakavuka Yordani.

⁶³ “‘Yohana, usisahau wakati Mungu alipowatembelea watu Wake nyikani kule, aliwaweka kwa muda wa miaka arobaini, na kila siku mwujiza ulitendeka. Yohana, tunaambiwa sasa ya kwamba siku za miujiza zimepita, lakini Yehova mkuu alitengeneza mkate na kuitiririsha juu ya nchi apate kuwalisha watu wetu kama milioni mbili na nusu, kwa muda wa miaka arobaini waliona mwujiza huo.’”

⁶⁴ Naye Yohana huenda alisema kitu kama hiki, tunapomsikiliza: “Ndugu, nimemwanguka wakati wote nilipokuwa nikimfuata, lakini leo hii nimeona kitu fulani. Nilikuwa nikimwuliza Mama, ‘Mama, ni wapi...? Je, Mungu ana ki—kikosi cha usiku kule juu ambacho, na matanuri makubwa huko juu Mbinguni kinachooka mikate hii yote, Malaika, kisha anaimwaga ardhini kwa ajili ya watoto Wake?’

“‘Mbona,’ akasema, ‘la, Yohana. Unajua, Mungu wetu anaweza kuumba mkate huo.’

“Sasa, daima nimeiamini hadithi hiyo, na leo hii, nilipomwona akichukua hiyo mikate mitano na kuwalisha watu elfu tano, hilo lilitosha.”

⁶⁵ Ninaweza kumsikia akigeuka, na kusema, “Mathayo, uliona mwonekano wa uso wake? Mbona, alionekana kana kwamba hakushangaa hata kidogo, mvulana huyo mdogo.”

⁶⁶ Mathayo akasema, “Naam, nilimwona. Kwa kweli, alikuwa ametoroka shuleni,” (vema, tulimwita “mtoro,”) “naye alikuwa ametoroka. Nami nikamwuliza...Ni—nikaangalia huku na huku, sikuona mtu pale aliyekuwa na chakula, bali alikuwa na chakula chake cha mchana mkononi mwake. Nami nikamwuliza kama ningeweza kukichukua, naye akasema, ‘Vema, nilikileta kwa ajili ya chakula changu cha kutwa, lakini kama kinapelekewa Mtu yule ambaye nimemsikia akinena, Yeye anaweza kukichukua.’”

⁶⁷ Ningependa tu kumsikia Yeye, nanyi je? kuona tu jinsi alivyokuwa tofauti. Nanyi mnaona, maadamu hicho chakula cha mchana kilikuwa mkononi mwa mvulana huyo mdogo, kilikuwa tu ni mikate mitano na samaki wawili, lakini kilipoingia

mkononi mwa Yesu, kiliwalisha elfu tano. Kwa hiyo vitu vidogo tulivyo navyo, kama tutamwacha tu avichukue, ile imani ndogo tuliyo nayo, kama tutamwachia tu, itafanya mambo makuu.

⁶⁸ Yohana alifurahi sana, akasema, “Alionekana kama Yehova, alipokuwa amesimama pale akichukua hizo biskuti na kuzivunja. Nami nikapanda hapo nyuma ya mwamba, nilitaka kuona mahali ulipotoka. Naye akaishika biskuti mkononi Mwake.” Na, ninasema “biskuti” kwa sababu sisi wakusini tunajua *biskuti* ni nini, mwajua. “Na kwa hiyo akaichukua biskuti hii na kuivunja, Naye, niliangalia kipande hicho kilichovunjwa, kisha akakitoa, ndipo alipoanza tena, kabla sijatambua, ile biskuti tayari ilikuwa imekua tena.”

⁶⁹ Akasema, “Katika mikono hiyo, hapana shaka ilikuwa imepakwa mafuta na mikono ile ile iliyofanya mkate ule huko juu Mbinguni na kuutuma chini. Nami, tuseme, ninatoa ushuhuda wangu kwenu ninyi ndugu, huku nje kwenye ziwa hili, usiku wa leo, ni jambo lililotatuliwa kwangu. Huyo ni zaidi ya mwanadamu, Huyo Ndiye, Ambaye—Ambaye manabii walitwambia habari zake.”

⁷⁰ Ndipo basi ninaweza kumwona Simoni, kama kawaida, mwajua, anataka kuingiza ushuhuda wake humo pia. Wala simlaumu, unapokuwa na kitu cha kushuhudia, inakubidi tu kutoa presha, hivyo tu. Kwa hiyo hapana shaka Simoni alisema, “Sasa, ndugu, wakati wangu umewadia.” Naye akasema, “Andrea, ndugu yangu, aliyeketi hapa mkono wangu wa kushoto, wakati aliposhuka kwenda kumsikiliza Yohana akihubiri. . . Loo, mwajua, jamani, tumesikia kila namna ya mambo, wala sikuyatilia maanani sana. Lakini usiku mmoja ha—hakuja nyumbani, nami nikashangaa alikaa wapi. Ndipo kesho yake asubuhi, huyu hapa anaingia, amekodoa macho, na kuniambia, ‘Njoo, umwone Mtu tuliyemwona, Masihi.’”

⁷¹ Alikaa Naye muda mrefu kutosha kushawishika. Hapo ndipo wengi wetu tunaposhindwa, kamwe hatukai muda mrefu vya kutosha kushawishika, hatuhusiki vya kutosha. Kuhusika, hii ni kati ya Uzima na mauti kwetu, kati ya kuwa mzima au kuwa mgonjwa. Nasi tunapaswa kukaa na kuangalia mpaka tutakaposhawishika, ndipo basi hakuna kitu kitakachotuzuia, wakati umeshawishika. Imani haina budi kuwa na kitu fulani cha kufanyia kazi, kutokea.

⁷² Na sasa, “Alipokuja akaniambia. . . Nami ninakumbuka ile siku niliyokutana Naye, nami nikasema, ‘Vema, nitaenda pamoja nawe mkutanoni. Yeye atakuwa huko chini ufukoni asubuhi ya leo, ulisema.’

⁷³ “Nami niliwaona maskini wavuvi wengi, wanawake wakipindua beseni zao za kuoshea juu chini, na kushuka kwenda kule ku—kumsikiliza Yeye. Naye Jamaa huyu alikuwa akivutia umati mkubwa sana wa watu, nami ni—nilifikiri

ningeshuka niende kule. Basi ni—nikajitwalia ki—kipande cha ubao uliochukuliwa na maji, basi nikawazia ningekeki tu chini, nisikilize, nikakaa huko nyuma kabisa.

⁷⁴ “Na wakati wote, alipokuwa akizungumza, ilionekana kana kwamba alikuwa akiniangalia moja kwa moja. Nami nikaendelea kuvutiwa zaidi wakati wote, nikaendelea kusogea karibu zaidi na mahali Yeye alipokuwa. Nami nikasema, ‘Vema, Yeye ananena Kimaandiko, inaonekana anajua kile anachozungumzia.’

“Ndipo kwa ghafla, akianiangalia moja kwa moja usoni mwangu, na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’”

⁷⁵ Akasema, “Ndipo nikashawishika,” kasema, “kwa sababu, Andrea, hapa atanishuhudia, mzee baba yangu, Mfarisayo halisi, naye alikuwa mtu mkali wa kidini. . . Na tulipovua samaki baharini hapa, nasi tungali tuna mtumbwi wake, naye alikuwa anazeeka, nami nikaona nywele zake zikiingia mvi, na uso wake ukiingia makunyazi, nilijua baba angetuacha hivi karibuni.

⁷⁶ “Kwa hiyo siku moja, aliketi chini baada ya sisi kuvua lundo kubwa la samaki, nasi tungeweza kulipa bili zetu wakati huo. Basi asubuhi hiyo, jinsi tulivyokuwa tumeomba, na kumwomba Mungu atusaidie, maana tuliwahitaji samaki hao *sana!* Basi tukawakamata hao samaki, ndipo Baba akaingia na kuketi chini, akasema, ‘Njoo hapa, Simoni, mwanangu.’

⁷⁷ “Akanikumbatia kwa mikono yake, kasema, ‘Simoni, ninazeeka, nami niliwazia siku zangu zote ya kwamba ningeishi nipate kumwona Masihi, bali ninazeeka, na labda sitaweza kumwona. Lakini huenda akaja katika wakati wako, Simoni.

⁷⁸ “Nami najua ya kwamba kabla ya kuja Kwake kutakuwako na mambo ya kila namna yakitukia, kutakuwako na manabii wa uongo, kutakuwako na kila kitu kikiendelea, kila namna za *itikadi*, kwa sababu itakuwa ni Shetani akijaribu kuwavuruga, na labda kuwadanganya Israeli.

⁷⁹ “Lakini, Mwanangu, kuna njia moja tu tunayoweza kuwa na hakika, na hiyo ni: dumu pamoja na Neno la Mungu, hiyo ndiyo njia pekee ya kuwa na hakika.” Huo ungekuwa ni ushuhuda mzuri mahali popote, hiyo ni kweli, “Dumuni na Neno.”

⁸⁰ “Ndipo akasema—akasema, ‘Mwanangu, katika lile Gombo, katika Kumbukumbu la Torati, Musa, yule aliyetupa torati, alisema, ‘Atakuja Masihi, Mmoja katika siku za mwisho, ama, Mungu atamwinua miongoni mwenu,’”” kuyathibitisha Maandiko, ““wa ndugu zetu, Naye atakuwa Nabii. Bwana, Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii.” Sasa, mwajua, tumeamriwa na Mungu kuwatii manabii, kwa sababu Neno la Mungu huwajia manabii, hao ndio walio na Neno na tafsiri ya Neno.

⁸¹ “Kwa hiyo, sasa Bwana wetu alitwambia kama kulikuwako na mmoja miongoni mwetu aliye wa kiroho, ama nabii, na kama alitabiri, na yale aliyosema hayakutimia, basi msimsikilize, lakini kama yalitimia, basi sikilizeni. Sasa, naye Masihi atakuwa nabii.’

⁸² “Na, kama ninyi ndugu mjuavyo, kwamba baba yangu ameondoka muda mrefu, lakini alipoangalia huko nje, na kuniambia mimi nilikuwa nani, na isitoshe Yeye alimjua maskini baba yangu mtauwa, nilijua Huyo alikuwa ni Yeye.” Ushuhuda mzuri sana, wa kushangaza.

⁸³ Basi kabla Simoni hajamaliza ushuhuda wake, Filipino alikuwa ameweka mikono yake begani mwake, akijaribu kumsimamisha kidogo. Unajua kila mtu hujaribu tu kuingia, na kumtangulia mwingine kidogo, mwajua. Umejaa *sana* hilo, unataka tu kusema jambo fulani. Naam. Unapomsikia mtu mwingine akizungumza, unataka tu kuingiza kitu fulani mle, hayo ni mazoea tu miongoni mwetu. Na kwa hiyo, unajua, Filipino, wakati wake wa kushuhudia ukafika, naye akasema, “Loo, jinsi ninavyokumbuka hilo! Nilikuwa nimesimama pale, nanyi mwajua, ilinichangamsha sana, hata . . . Nathanaeli, hujali nikilisimulia?”

“La, hilo ni sawa.”

⁸⁴ “Unajua, nilijua Nathanaeli alikuwa mwaminio halisi, wa kiothodoksi. Alishika torati yote, naye alikuwa ni mtu mwema, alikuwa ametumika wakati wake kama mzee, naye alikuwa amefanya mambo yote mbalimbali, naye alikuwa ni mtu mzuri. Alisoma katika Maandiko usiku na mchana, najua alikuwa amefunzwa vema, naye alikuwa ni rafiki yangu msiri. Kwa hiyo nikaenda mbio kuzunguka kilima kwa nguvu nilivyoweza kumtafuta Nathanaeli. Vema, mnajua, enyi ndugu, inanichukua kama siku moja kutoka mahali alipokuwa akihubiri pale, kukizunguka kilima. Na—nami nikaona. . . Kwanza nilibisha mlango, naye Ndugu Nathanaeli, mke akaja mlangoni na kusema, ‘Ametoka tu kupitia kwenye kichaka chake.’ Nami nikaenda huko nje, nami nikamsikia mtu fulani akiomba.

⁸⁵ “Na—naye Nathanaeli alikuwa amepiga magoti akiomba Mungu amtume Mkombozi, kama alivyomtuma Musa. Basi alipomaliza, nilijua ya kwamba alikuwa katika hali ya namna hiyo, akimtafuta, kwa hiyo nikasema, ‘Njoo, uone Yule tuliyemwona. Sisi. . . Maombi yako yamejibiwa. Kile kitu ulichokuwa ukitafta tayari kipo hapa. Naam, Bwana. Tumekiona, ni kizuri sana! Yakupasa uje, uone.’

“Naye Nathanaeli akasema, ‘Ni nini hilo unalosema?’”

Naye akasema, “‘Tumemwona, Ambaye Musa na torati ilisema yuaja, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.’

⁸⁶ “Na sasa, Nathanaeli, mwajua, alikuwa mwaethodoksi mwaminifu, akasema, ‘Sasa, hebu kidogo, Filipino, nakujua wewe

kama m—msomi mzuri wa Biblia, hapana shaka umeingia wazimu mahali fulani. Laweza neno jema kutoka Nazareti?”

87 “Mnajua, sikupoteza maneno yangu, kwa sababu hakuna haja ya kubishana na mtu yeyote, kwa hiyo nikamwambia tu, ‘Njoo, uone.’ Basi tulipokuwa tukija, yeye alisema, ‘Kwa nini umeshawishika sana?’

88 “Nami—nami nikamwambia Nathanaeli, huku nikimkumbatia, ‘Sasa, Ndugu Nathanaeli, unajua ni mara ngapi tumeketi kwenye mashua, nasi, tumeyajadili hayo Magombo mchana na usiku, jinsi tulivyokesha sana, nasi tumeyasoma Maandiko,’” loo, hilo ni zuri sana, “‘jinsi tumeyasoma Maandiko pamoja, na—na haya ndiyo yaliyonisadikisha: Je, mnajua ya kwamba. . .?’ Petro, je, utanisamehe nikilisema?”

“Hakika, endelea.”

“Unajua yule mvuvi asiye na elimu ambaye sikuzote alikuwa taabani, kisha akanunua samaki chini kule?”

“Loo, naam. Mwana wa Yona, Simoni?”

89 “Naam, huyo ndiye. Nawe wajua, ulinunua samaki kutoka kwake siku moja na mkataka risiti, wala hata asingeweza kuandika jina lake humo, hakujua kiasi hicho.’

“Naam, ninamkumbuka. Naam, ana ndugu wanayemwita, ‘Andrea.’”

90 “Naam, huyo ndiye. Um-hum. Naam. Vema, Andrea aliamini Nabii huyu kuwa ndiye Masihi, naye akaja, akamchukua Petro, ama, Simoni, kisha akamleta kwa Yesu, ndipo Yesu alipomwangalia usoni, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Hakuja lolote kumhusu.’

91 “Sasa, Nathanaeli, hebu nikukumbushe jambo hili: Hivi torati haikusema, ‘Nabii akitabiri. . .?’ Na miaka mia nne tangu wakati huo hatujawa na nabii, na Hili hapa moja kwa moja mbele zetu. Mnajua, mbona, halingenishangaza, Filipino, kwamba kama Yeye hakukwambia wewe ni nani, ama, Nathanaeli, ulipofika pale.’

92 “Vema, sitakuwa wa kupinga,’ akasema Nathanaeli. ‘Nitapanda tu juu, na nisikie mwenyewe na kutoa maamuzi yangu mwenyewe. Na kama Yeye ni wa Kimaandiko, ninajua yale Biblia isemayo juu yao, na kama linasikika la Kimaandiko, mbona, sina budi kuliona likifanywa kwanza, mimi, kama ninaweza kuliona likitendeka, basi nitaliamini.’

93 Vema. Hilo ni zuri sana. Unajua, wote hawaishi Missouri. Ulisikia ule msemu wa kale, “Ninatoka Missouri, nionyeshe.”

94 Kwa hiyo, akasema, “Alikuwa, ndipo siku hiyo, tulipofika kule, kulikuwa na mstari wa maombi, na kulikuwa na watu waliosimama kwenye mstari wa maombi, naye Yesu alikuwa akiwaombea wa—wagonjwa. Basi nilipokuja pamoja na

Nathanaeli, tuliona kundi la marabi wamesimama huko nje, na makasisi wakuu, mashuhuri.

⁹⁵ “Basi tulipopita, tulisikia maongezi yao, ndipo mmoja wao akasema, ‘Vema, mnajua inatubidi kulijibu kusanyiko letu. Na kama wote wakianza kulikimbilia *hilo*, tutafanyaje? Vema, tumeona yale aliyofanya muda mfupi uliopita. Alijuaje mambo hayo? Kwa hiyo itatubidi kufanya baraza sasa, tuone yale itatubidi kulijibu kusanyiko letu Jumapili ijayo, watakapoulizia jambo hili. Na, mwajua, hatuwezi kumwamini.’

⁹⁶ “Kwa hiyo wakasema, ‘Tutasema tu kwamba yeye ni Beelzebuli, mkuu wa pepo, yeye ni mpiga ramli, hiyo ndiyo njia bora zaidi tunayoweza kufanya jambo hilo.’” Mnaona, badala ya kuketi chini, na kuyachunguza Maandiko, wanatoa tu maoni yao wenyewe, yale wanayowazia.

⁹⁷ “Walipokuwa wakifanya hayo Yesu aligeuka na kujua mawazo yao, Naye akasema . . .” Mnakumbuka? Biblia ilisema hawakulinena kwa sauti kubwa, waliliwazia moyoni mwao, ndipo Yesu akalishika. Sawa. “Ndipo alipowaambia ya kwamba angewasamehe hilo, lakini itakuja siku nyingine, wakati fulani, ambapo Roho Mtakatifu angekuja . . .

⁹⁸ “Sasa, bado hatuelewi hilo, enyi ndugu katika meli hii, usiku wa leo, mwajua, vipi kuhusu huyo Roho Mtakatifu anayemmena kuja. Lakini Yeye alisema wakati atakapokuja na angefanya jambo lile lile, kwamba kuna neno dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe. Basi, ndugu, hapana shaka kuna kitu fulani mbele ambacho Yeye anajiandaa kufanya kulifanya hilo gumu sana, hapana shaka ni jambo kubwa sana.

⁹⁹ “Sasa, basi wakati Ndugu Nathanaeli alipokuwa amesimama pale, Yesu aligeuka na kumtazama na kusema, ‘Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake!’ Nawe je, unakumbuka, Nathanaeli? Lilikushangaza mno.

¹⁰⁰ “Nawe ukageuka, kisha ukaangalia kando, na huyo hapo amesimama askofu wenu, ama, rabi wenu, akisimama pale kwenye baraza hilo, naye akaangalia chini na kukuona, ‘Ahem!’ akasafisha koo lake, kwa sababu ulichangia sana kanisani.

¹⁰¹ “Lakini basi, ilikuwa ni kuchagua kati ya yale rabi alikuwa amesema, ama yale Mungu alikuwa amesema, kwa hiyo ukageuka ukamwita Yesu, ‘Rabi, Mwalimu, ulinijuaje Wewe? Sijawahi kukuona wala Wewe hujawahi kuniona. Kwa hiyo ungejuaje ya kwamba nilikuwa mwa—mwaminio mwaminifu wa kiothodoksi?’

“Nawe unakumbuka, Nathanaeli, aliyosema?”

Nathanaeli akasema, “Naweza kulisema?”

“Naam.”

¹⁰² “Akasema, ‘Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti nalikuona.’” Nathanaeli akasema, “Sitaki kuukatiza ushuhuda

wako, lakini hilo lilitosha kwangu. Hebu niwaambie hawa ndugu yale niliyosema, sijali kama ninii, watu wote mashuhuri walikuwa wamesimama hapo, nilimwendea mbio na kusema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’” Kwa sababu lilikuwa ni la Kimaandiko, yeye alilijua. “Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

¹⁰³ Maskini Andrea mvumilivu, alikuwa amengojea muda mrefu sana kwa ajili ya ushuhuda wake. Na, lakini Nathanaeli... Ndipo kila mtu alijua mwezi ulikuwa unachomoza. Na kwa hiyo, huo mkutano wa ushuhuda, mwajua, wakati mkutano mzuri wa ushuhuda unapoanza, mbona, wa—wananinii tu, kamwe hujui muda unapokwisha, unazidi tu kusonga mbele. Kwa hiyo, loo, walivutiwa sana, kila mmoja akisikiliza ushuhuda wa mwingine.

¹⁰⁴ Ndipo Andrea akasema, “Ndugu, hebu sote tuwazie jambo hili, kwa kuwa tunazunguza juu ya huduma Yake, kama ni pamoja na Neno la Mungu ama la, sote tunajua hilo. Hebu niwakumbushe: Mnakumbuka siku ile Yeye aliposema, ‘Nitawapeleka ninyi nyote Yeriko?’ Sote tunajua hilo.” Naye Andrea lazima alisimama, akaitikisa hiyo mashua kidogo labda, akanyamaza katika dakika moja.

¹⁰⁵ Naye akasema, “Ninyi nyote mnakumbuka tuliposhuka, tulipokuwa tukienda Yeriko, na kesho yake asubuhi, ilikuwa ni ajabu, baada ya sisi kuamka na kuvaa majoho yetu tena, Naye akasema, ‘Nina haja, kupitia Samaria.’ Tulifikiri hilo lilikuwa ni jambo geni, jinsi ambavyo angezungukia huko Samaria, badala ya kwenda moja kwa moja hadi Yeriko.

¹⁰⁶ “Nasi tukatembea, nanyi mnakumbuka, tuliondoka bila kiamshakinywa, ndipo tukaona njaa. Ndipo yapata saa tano mchana, tukaja kwenye mji huu unaoitwa Sikari, ndipo sisi—sisi tukaketi pale karibu na kisima, naye akatutuma sote, nasi tukashuka kwenda mjini. Mnakumbuka, ni wakati wa jinsi gani, waliposema, ‘Je, ninyi ni mmoja wa hao watakatifu wanaojibingi-... , ama, ninyi ni mmoja wao?’” Kwa hiyo, samahani, sikupaswa kusema hivyo, labda. Mnaona? Lakini, “Je, ni—ninyi ni mmoja wao pamoja na kundi hilo la Wagalilaya huko nje? Ninyi ni mmoja wao? Na kwa hiyo, hata wasingetupa chakula. Loo, jamani, ilikuwa mbaya. Nasi tukarudi tena kisiri.

¹⁰⁷ “Ndipo tukaona jambo la kigeni, kulikuwako na kijana mwanamke mrembo, akielekea kisimani, huku mtungi wake wa maji umewekwa begani mwake, kichwani mwake. Naye alipopanda juu, tulimwona akiweka huo mtungi chini, na kuweka kulabu ndani yake, akiwa tayari kushusha winchi, nasi tukaona ya kwamba Bwana wetu alikuwa ameketi huku ameinamisha kichwa Chake. Tuliyaona macho Yake wakati yalipoinuliwa, nasi tukaona ya kwamba alikuwa ametiwa alama kama kahaba, sifa mbaya. Asingekuwa nje kwenye pampu wakati huo wa mchana, wanawali wanatoka mapema, kwa hiyo

basi, tulijua ya kwamba alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya.

¹⁰⁸ “Nasi tuliwazia tu, mwajua, kila mmoja wetu alisema, ‘Hebu tumwone Yeye akimfukuza kutoka kwenye kile kisima.’ Mnakumbuka jinsi tulivyokuwa wa kimwili, ndugu? Tunamwona tu Yeye akimfukuza kutoka kwenye kisima hicho. Kwa hiyo tukajificha vichakani. Nyote mnakumbuka hilo?”

“Naam. Amina. Tunakumbuka jambo hilo. A-ha.”

¹⁰⁹ “Nasi tulikuwa tunaenda kumwangualia Bwana wetu akimfukuza mwanamke huyu mwenye sifa mbaya kutoka Uweponi Mwake. Kwa hiyo akaanza kushusha bi—birika la maji, chini kuchota maji, ndipo Bwana wetu akamwambia, ‘Mwanamke, nipe maji ninywe.’ Jamani! Mnakumbuka jinsi tulivyotazamana? Hilo lingekuwa ni jambo la kushangaza, jinsi ambavyo mwanamke wa aina hiyo angeweza kuombwa kumfadhili Bwana.”

¹¹⁰ Lakini mnajua, Mungu hufanya kazi katika—katika njia za siri, Yeye anawapenda walio waovu sana kati yetu. Kama hakuwapenda, ni—nisingekuwa hapa usiku wa leo. Nami nina hakika sote tunajisikia hivyo. Naam.

¹¹¹ “Na wakati... Alishangaa, akaangalia kote, akasema, ‘Bwana, Wewe ni Myahudi, nami ni mwanamke Msamaria, wala hatuna uhusiano wowote sisi kwa sisi. Kwa nini unizoe, uniulize swali kama hilo?’

¹¹² “Naye akasema, ‘Mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.’ Nasi tukashangaa, ‘Alikuwa akijaribu kufanya nini?’ na ‘Kwa nini alikuwa akijaribu kumtumia mwanamke kama huyu kufanya jambo fulani naye?’ Kasema, ‘Kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, ningekupa maji ambayo isingekubidi kuja hapa kuteka.’” Loo, jamani! Laiti... Hivi huna furaha kwamba umepata mwaliko uo huo?

“Nasi sote tukashangaa, tulipokuwa tumesimama tukijificha vichakani... Mathayo, unakumbuka? Uliandika hilo.”

“Loo, naam, ninalo, usijali.” Ninalisoma usiku wa leo, mnaona.

Kwa hiyo akasema, “U—uliandika hilo?”

“Naam.”

“Nasi sote tulikuwa tumejificha huko nyuma vichakani.”

“A-ha.”

¹¹³ “Na ninii... waliingia katika mazungumzo, na, kuhusu mahali ambapo watu wanapaswa kuabudia.” Nanyi mwajua, wangali katika mazungumzo hayo, mmoja alisema, “Inakubidi kuabudu katika kanisa la Kimethodisti.”

Huyo mwingine akasema, “Kanisa la Kibaptisti.”

Mwingine akasema, “Kanisa Katoliki.”

Na huyo mwingine akasema, “Kanisa la Kipentekoste.”

114 “Lakini unajua kile Yeye alichosema? ‘Waabuduo wa kweli humwabudu Yeye katika roho na kweli, naye Baba anawatafuta watu kama hao.’ Nasi tulishangaa basi, kile alichokuwa akijaribu kufanya, lakini sasa tunaelewa, Yeye alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake. Tukatambua basi kwa nini alikuwa na haja ya kwenda juu. . .

115 “Mnajua, wakati mmoja Yeye alitwambia, wakati alipomfufua Lazaro kule juu, akasema Baba alikuwa amemtuma. Nanyi mnakumbuka alimwambia mtu yule kwenye—kwenye. . .siku ile, wakati Yeye. . .wote walipokuwa wakijaribu kuyagusa mavazi Yake, naye akapitia kwenye umati huo mkubwa kule kwenye bi—birika la Bethesda, Naye akageuka na kuwaambia, ‘Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda?’ Kwa hiyo tunaelewa sasa, lakini basi. . .

116 “Na ndipo tuliona ya kwamba, ya kwamba huyo mwanamke alikuwa akipata. . .akiketi, loo, kisimani, bado ameshika huo mtungi mkononi mwake, apate kuteka maji, ndipo Yeye akamwambia, ‘Mwanamke, nenda kamwite mumeo mje naye hapa.’ Nawe unajua ulichosema wakati huo, Bartholomayo? ‘Alijuaje alikuwa na mume?’

117 “Ndipo huyo mwanamke akashangaa, na nywele za—zake nzuri zikaanguka usoni mwake, nayo macho yake makubwa, maangavu yakametameta, ndipo akasema, ‘Bwana, sina mume.’ Nasi sote tukawazia, ‘Loo, jamani! Kuna kasoro sasa.’

118 “Ikatushangaza, Yeye alisema, ‘Umesea kweli.’ Ndipo tukashangaa, sivyo, ndugu? Hatukujua. Akasema, ‘Kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.’

119 “Sasa, tulishangaa ni mjibizo wa namna gani uliokuwa ukitoka kwenye hili. Naye akamwangalia moja kwa moja usoni Mwake na kusema, ‘Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.’” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

120 Na yapata wakati huo Nathanaeli akasema, “Naam, niliwazia jinsi ilivyokuwa tofauti na rabi wetu, alionekana kujua zaidi kumhusu Mungu kuliko rabi alivyomjua, kwa sababu alisema Yeye alikuwa ni ibilisi. Inaonekana kana kwamba huyo mwanamke, tulijua wakati huo, alikuwa akiyasoma Maandiko, tulishangaa atasema nini tena.”

121 “Yeye akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.’ Nasi tukaangaliana, ‘Mwanamke wa namna hiyo? Hakika amekuwa akisoma yale magombo, na hata hivyo, yeye si Myahudi.’ Angalia kile anachosema sasa: ‘Tunajua ya kwamba Masihi, anayeitwa Kristo, Yeye yuaja, Naye atakuwa ni Nabii, kwa sababu Musa

alisema hivyo, atakapokuja, atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe? Hapana shaka Wewe ni nabii.’

“Yesu akasema, ‘Mimi ninayesema nawe, Ndiye.’

¹²² “Nanyi mnakumbuka? Hapo akaangusha mtungi huo, akaelekea mjini upesi alivyoweza kwenda, akipaza sauti, ‘Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Sasa, ninyi watu mnaoamini, kuyasoma Maandiko, hivi Maandiko hayasemi ya kwamba hiyo ndiyo ishara ya Masihi?’”

¹²³ Sasa, hebu nisimamishe huo ushuhuda, nishuke nije hapa kwa dakika moja, hapa—hapa Columbia. Mliona? Kamwe hakufanya hivyo mbele ya yeyote wa Mataifa, ni Wayahudi tu na Wasamaria. Hiyo ni kweli. Na kuna jamii tatu tu za watu duniani, kama unaamini Biblia yako, hao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, huko ndiko sote tulikotokea; Myahudi, Msamaria, na Mmataifa.

¹²⁴ Nao Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, Yeye aliwaonyesha kile Masihi alichokuwa, Nathanaeli, Petro, na hao wengine, wanathibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake. Nao Wa—Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi, Naye akawaonyesha papo hapo kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Lakini Mataifa, sisi, tulikuwa tukiabudu sanamu wakati huo, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote.

¹²⁵ Ningetaka kuuliza hili—kuuliza swali hili usiku wa leo, wakati tukinirii. . . ndipo tuta—tutafungua skrini yetu tena, lakini wakati tukiwa hapa: Mataifa, sasa, huo ulikuwa ndio mwisho wa Wayahudi, na sasa wakati wa Mataifa unakwisha. Na kama tunamtazamia Masihi ajaye, nasi tunaamini ya kwamba katika umbo la Roho Mtakatifu, Yeye yupo hapa, nayo Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Waebrania 13:8, na kama hiyo ilikuwa ndiyo alama ya utambulisho katika siku hizo, na Masihi huyo alisema katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nifizanyazo Mimi yeye naye atazifanya,” Naye akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. . .” Mliona jambo hilo?

¹²⁶ Usiondoe hizo tatu niani mwako, kama vile kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, namba hizo zote za ukamilifu; Kuja kwa kwanza kumkomboa Bibi-arusi Wake, Kuja mara ya pili kumnyakua Bibi-arusi Wake, mara ya tatu, akija pamoja na Bibi-arusi Wake, mnaona, hizo tatu zo—zote, kote katika Biblia.

¹²⁷ Sasa, liangalieni kwa makini, kuna matabaka matatu ya watu, hayo ni, waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Na mwishoni, wakati. . . Kuna makanisa matatu ambayo watu hawa watatu ni wafuasi wake: Ibrahimu

aliwakilisha Kanisa teule, Lutu aliwakilisha kanisa baridi ulimwenguni, lakini basi Wasodoma waliuwakilisha ulimwengu.

¹²⁸ Nao Malaika watatu wakamjia Ibrahimu. Wawili wao walishuka, na kuihubiri Injili na kujaribu kumwita Lutu na watu wake watoke, wakijaribu kupata hata watu kumi waliokuwa wenye haki. Lakini Mmoja alibaki nyuma, na Yule aliyebaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu, na Kanisa teule. . . Ninaamini Kanisa limeteuliwa, ni kwa kujua kwa Mungu tangu zamani, limekusudiwa tangu zamani, kwa sababu Yeye huchagua tangu zamani kwa kujua tangu zamani, mnaona. Kanisa hilo litakuwako, sasa, niweko au nisiweko, sijui, sina budi kutimiza wokovu wangu. Lakini—lakini ninajua Kanisa litakuwako, hiyo ni kweli, ninatumaini tu mimi ni sehemu Yake. Nami ninaamini, mradi mimi ni sehemu Yake, nitakuwa kule pamoja Nalo. Hapo ndipo tumaini langu linapotulia, papo hapo.

¹²⁹ Na sasa, hapo, Lutu alihubiriwa Injili, na ninii zake. . . dhambi za mji huo ziliitesa nafsi yake yenye haki kila siku. Na wakati alipowaona hawa akina Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, wakija, kulikuwa na kitu kilichomgusa, alijua ya kwamba hao walikuwa ni zaidi kidogo ya mtu wa kawaida. Hawakufanya miujiza mingi, waliwapofusha tu baadhi ya watu usiku mmoja, na—na kuihubiri Injili humpofusha asiyeamini, hiyo ni kweli.

¹³⁰ Lakini Malaika huyu aliyekaa na Kanisa teule, Ibrahimu na kundi lake, aliketi huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Naye Sara, alikuwa tofauti kidogo na baadhi ya dada zetu wa kisasa siku hizi. Mnajua, hivi haikufanyi ujisikie vibaya wakati, unajua, wanaume wakianza kuzungumza, nao wanawake wanatoka na kuingilia moja kwa moja, na, loo, kidogo ni fidhuli? Wao. . .

¹³¹ Mnajua, wakati Mungu alipomwumba mwanamke, alimpa roho ya kike kuwa mrembo na wa kuvutia, kama walivyo dada halisi Wakristo. Lakini wanawake hawa waliovaa ovaroli, sigara mdomoni mwao, na kukanyagakanyaga na kulaani, na kuimba, *Mungu Ibariki Marekani*, mnaona. Na hiyo—hiyo, haionekani kabisa. . . inaonekana ni fidhuli. Kamwe haininii. . . Kuna kasoro fulani, mnaona. Hiyo ni kweli, mnaona. Na, lakini maskini Sara alikuwa maskini dada Mpentekoste aliyebaki nyuma na kushughulikia kazi yake, alikuwa huko nyuma akipika chakula cha kutwa, mnaona.

¹³² Na kwa hiyo, Malaika aliyeketi pale alikuwa akimwangalia Ibrahimu. Sasa, kumbukeni jina lake lilikuwa ni Abramu siku moja tu kabla ya hapo, kabla yake tu, wala Sara hakuwa *Sara*: Sara, S-a-r-a-i, nalo likabadilika likawa S-a-r-a, na A-b-e-r-h-a-m-u; *Ibrahimu*, “baba wa mataifa,” na *Sara*, “binti mfalme.” Kwa hiyo huyu alikuwa ni Mtu wa ajabu, alikuwa na mavumbi

nguoni Mwake, alikuwa tu amevaa kama mtu wa kawaida, Naye akasimama pale, na kusema, “Ibrahimu. . .”

¹³³ Sasa, Yeye alikuja tu na kuketi chini, Ibrahimu akatoka na kumkaribisha ndani, Yeye, mtu wa kawaida tu, akaanza kupita, akasema, “Karibu, keti, nitachota maji kidogo, na kutawadha miguu Yako. Na—nami nitakupa kipande cha mkate, kisha uende Zako.” Ibrahimu, ninaamini, kidogo aliwazia kulikuwa na kitu cha kigeni pale. Mnaona? Loo, kuna jambo fulani kulihusu, unaweza tu kulihisi, anapokuja karibu. Unaweza tu kujua wakati unapozungumza Naye. Unaona?

¹³⁴ Kasema, “Keti.” Naye akachukua kichaka cha nzi na, ni wangapi wenu ninyi watu wa kusini mngali mnajua kichaka cha nzi ni nini? La? Mashindano ya mbio yanafifia. Mbona, kamwe hatukuwa na mlango wa skrini mpaka hivi majuzi tu. Naye alikuwa na maskini kichaka cha nzi huko nje, mwajua, na kumwangukia akila. Naye akamchinja ndama, kisha akamlisha Mtu huyu mkate ambao Sara alikuwa ameoka, na vipande vya nyama ya ndama, naye alikuwa na maziwa, akaketi pale na kula, naye akawafukuza nzi walipokuwa wakila.

¹³⁵ Na kwa hiyo akaendelea kuangalia kuelekea Sodom, ndipo akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Whiu! Wanaiita telepathia siku hizi, ninamaanisha, jina la kisasa wanalotaka kuliita. Hivyo ndivyo walivyosema Yesu alikuwa, “Beelzebuli, mpiga ramli.” Hiyo ingekuwa ni telepathia ya namna gani?

¹³⁶ “Ibrahimu,” akamwita kwa jina lake la kitaifa, ama, kimataifa, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Binti mfalme! Liangalieni, jinsi linavyoendelezwa. Na sasa kumbukeni, Maandiko yalisema alikuwa kwenye hema nyuma ya yule Mtu. Naye akasema, “Ibrahimu. . .”

¹³⁷ Bila shaka, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja papo hapo, naye Sara alikuwa na tisini, kwa hiyo wote wawili walikuwa na umri mkubwa. Maskini Sara kama maskini bikizee, mwajua, na—nao walikuwa wameahidiwa mtoto huyu mchanga, naye alikuwa akimngojea, naye Ibrahimu akiwa na ndevu zilizing’nia chini kabisa, ameinama, mwajua, kwenye fimbo yake.

Akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Ndipo Ibrahimu akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

¹³⁸ Akasema, “Ibrahimu, Mimi,” napenda hilo. *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, kwa hiyo. . . “Nitakurudia, kulingana na majira ya uhai,” ambalo alikuwa ameahidi. Sasa mnaona Huyo alikuwa ni Nani.

¹³⁹ Naye Sara, kwenye hema, mwajua, tunakuita siku hizi, “kucheka kifichifichi,” mwajua, akasema, “Mimi, nikiwa mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka tisini, na bwana wangu,” ambaye alikuwa ni mume wake, “huko nje ni mzee,

umri mkubwa.” Mbona, kama mume na mke, labda hawakuwa kama mume na mke kwa muda wa miaka kumi, ishirini. Na kuwazia, “Mimi, mwanamke mkongwe, na mume wangu, mzee, ati tutakuwa na raha pamoja kama vijana?” Naye akacheka kimoyomoyo.

¹⁴⁰ Ndipo yule Malaika akasema, ama, huyo Mtu akasema, “Kwa nini Sara akacheka hemani, akisema mambo haya hayawezekani?” Akajaribu kulikana, bali Yeye akasema, “Naam, ulicheka.”

¹⁴¹ Sasa, hebu niingize muhtasari m—mdogo papa hapa, Natumaini ninyi watu mnalipata, ninyi watu mnaoamini katika, neema ya Mungu, papo hapo Mungu angalimwua mwanamke huyo, kwa kutokuamini kwake, asingejipumbaza naye dakika nyingine. Huyo, Huyo alikuwa ni Mungu, Mwenyewe. Sasa, soma, uone kama ni . . .

¹⁴² Unasema, “Ilikuwa ni mwanadamu.” Unasema, “Je, Mungu angeweza kula nyama, na Mungu afanye *hivi*?” Kweli kabisa. Ibrahimu alizungumza Naye na angalieni kama si Elohimu. Mungu alijitambulisha Mwenyewe katika mwili wa nyama na kufanya ishara.

¹⁴³ Na sababu ya Mungu kutouchukua uhai wa Sara: Asingeweza kufanya hivyo, kwa kuwa alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu, naye Ibrahimu alikuwa na ahadi. Loo! Mnalipata? Loo, jamani! Basi Yeye hawezi kutuchukua, sisi ni sehemu ya Kristo. Mnaona, ingembidi kumchukua Ibrahimu pia, maana hiyo ni sehemu ya Ibrahimu. Basi wakati Yeye . . . Sisi ni Bibi-arusi wa Kristo, ndivyo lilivyo Kanisa, na halafu, kile kilicho ndani ya Kristo, sisi ni sehemu Yake. Naye akasema ya kwamba asingeweza kufanya hivyo.

¹⁴⁴ Naye akasema, “Naam, ulicheka.”

¹⁴⁵ Sasa, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Ilikuwa ni kitu gani? Mungu, Yehova, akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Na sasa, Roho Mtakatifu, Mungu, katika siku za mwisho, kabla tu ya yale maangamizi ya kuiteketeza dunia kwa moto, kama vile alivyokuwa akienda kuiteketeza dunia huko Sodoma, tuna wainjilisti wa kisasa wanaoenda kote duniani katika kanisa la kawaida, naye Roho Mtakatifu amekuja akaingia katika mwili wa mwanadamu, Kanisa, hiyo ndiyo ishara kwa Mataifa.

¹⁴⁶ Hebu turudi Galilaya kwa dakika moja tu. Loo, ni wakati wa jinsi gani waliokuwa nao! Ninaamini wote walikuwa wakipiga makelele, “Amina,” pia. Halafu basi, tungeweza kumwendea, loo, Bartimayo, jinsi ambavyo Yesu, akipanda kwenda kule Kalvari, akitoka Yeriko, naye Bartimayo, maskini ombaomba huyo akiwa ameketi pale, na, mbona, Yeye kamwe asingeweza kumsikia, kwa kawaida.

147 Mbona, kulikuwako na maelfu ya watu wakimfuata, wakipiga makelele, “Aisee, wewe unayeweza kuwafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, hebu tukuone ukija kuwafufua.” Wakimtupia matunda yaliyooza, na kila kitu. Uso Wake umeelekezwa Kalvari, Yeye alikuwa akienda.

148 Lakini maskini huyo ombaomba labda akijua huenda... Huenda msichana fulani Mkristo alipita, na maskini huyo jamaa, walikuwa wakimkanyagia chini, naye akasema, “Mama, niambie ni Nani anayepita hapa? Vurugu hizi zote ni za nini?” Ni ajabu, alipo Yesu, kuna vurugu nyingi, kelele, mmoja akimwunga mkono, mmoja akimpinga.

149 Kwa hiyo wa—wao wanaona ya kwamba msichana huyu alisema, “Mbona, Bwana, mimi ni mfuasi wa huyu Nabii kijana. Wewe ni mwaminio wa Maandiko, sivyo?”

“Loo, hakika.”

“Vema, hivi hujui...? Hivi uliwahi kuisoma Biblia, kabla hujapoteza macho?”

“Mara nyingi.”

“Je, unamjua, Mwana wa Daudi?”

“Naam, anapaswa kuja.”

“Hapo, amepitia hapa hivi punde tu.”

150 Ndipo hapana shaka Bartimayo alisema, “Ikiwa Huyu Ndiye, sauti yangu, mimi ni dhaifu na mzee, jambo pekee ninaloweza kufanya ni kusema, ‘Yehova, unirehemu.’ Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

151 Ndipo imani ya huyo ombaomba ikamsimamisha, kama tu yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu alivyomsimamisha kwa mguso wa imani yake. Imani ya huyo ombaomba ikamsimamisha, Naye akasimama kimya. Ningependa kuhubiri juu ya jambo hilo, kesho usiku: *Ndipo Yesu Akasimama Kimya*, vema, Bwana akipenda.

152 Sasa, angalieni, Naye akasimama na kumwita, na kusema, “Unataka nifanye nini?”

153 Ninaweza kumkumbuka Zakayo juu ya mti. Naye alipanda kule kujificha, mwajua, akasema, “Loo, mimi ni mfanyabiashara hapa mjini, kamwe nisingejichanganya na kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha,” nawasikia wakija, “kwa hiyo nitapanda juu ya mti huu, ndipo atakapopitia hapa nitatoa maoni yangu juu Yake.”

154 Huyu hapa anakuja akitembea moja kwa moja chini ya huo mti, mwajua, akasimama, kasema, “Zakayo, shuka chini,” huku ameketi huko juu amejifunika majani, kusudi mtu yeyote asimwone. Lakini Yeye anajua tu mahali ulipo, huenda ukavuta majani ya Kimethodisti, na majani ya Kibaptisti, na kujifunika

kila namna ya majani, bali Yeye anajua papo hapo ulipo, usiku wa leo.

¹⁵⁵ Walipokuwa... Loo! Walipokuwa huko nje... Tutaharakisha ushuhuda kisha tuwaombe wagonjwa. Hebu na tuangalie kwa dakika moja tu, turudi nyuma, nyuma zaidi kidogo, hebu turudi nyuma sasa, ni, wao walisema, “Loo, Mungu asifiwe!” Wote walikuwa wakipiga makelele, na wakiwa na wakati mzuri sana.

¹⁵⁶ Ndipo upepo mdogo ukavuma. Ilikuwa ni kitu gani? Hapana shaka Shetani aliangalia juu kutoka juu ya jangwa hilo, kilima kikavu, naye akawazia hivi: “Hao hapo, nao wameondoka bila Yeye, sasa ni nafasi yangu.”

¹⁵⁷ Hilo ndilo analotaka, kulipata Kanisa. Mwajua, juzijuzi tumekuwa na shughuli nyingi sana kwa vyovyote vile, mwajua. Kumekuwa na uamsho kote nchini, kwa namna fulani umepungua sasa, mioto inazima. Lakini tumekuwa na shughuli nyingi sana, kuunda madhehebu mapya na mihemuko mipya, nami nashangaa kama hatuondoki wakati mwingine bila Yeye. Mnajua, Yeye ni Neno, kweli, Neno. Dumuni na Neno. Mungu anaweza kufanya lolote atakalo, lakini kwangu mimi, ninii tu, Yeye ni Neno, mradi liko katika Neno *Hapa*, basi ninaliamini. Mnaona?

¹⁵⁸ Kwa hiyo tumekuwa tukikimbia *hapa* na *pale*, na kukimbilia kila kitu, lakini mimi—mimi—mimi... labda huenda tulimwacha mahali fulani. Kwa hiyo mara ibilisi anapoliona kanisa bila Kristo... Mwajua, ni vibaya sana, nimeninii... Karibu nihubiri juu ya hilo, lakini ni wengi wetu sana tunaovipenda vipindi vya televisheni, badala ya mkutano wa maombi ya Jumatano usiku, basi tu—tunaninii tu, kwa namna fulani tunaondoka bila Yeye. Tulipata pesa nyingi sana, ndipo tukaanza kuwazia kuhusu mavazi, na dada zetu wote wanakata nywele zao, na kuzunguka-zunguka, kwa namna fulani tuna *mtindo*, tukiyaangalia makanisa mengine, nami... labda tunaondoka bila Yeye. Mnaona?

¹⁵⁹ Kwa hiyo ibilisi akasema, “Sasa ni wakati wangu wa kuwakamata.” Hapo ndipo anapolenga hiyo shabaha kali. Kwa hiyo wanaenda bila Yeye. Kwa hiyo akasimama juu ya kilima, naye akaanza kuwarushia pumzi yake, “Nitawazamisha.”

¹⁶⁰ Ndipo maskini jamaa hao wakaanza kuvuta, wakajaribu kutwika matanga, nao upepo ukayakata hayo matanga. Nao wakajaribu kuvuta kwa makasia yao, nayo yakavunjika. Wakajaribu kujiunga na kanisa moja kisha lingine. Muda si muda mwajua, maskini jahazi lao wenyewe likajaa maji.

¹⁶¹ Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Hmm, hmm, hmm! Loo, na—nawaambia ni, Yeye ni mkuu. Nami nafikiri majahazi mengi madogo yanajaa maji, lakini mwajua, wanakuta ya kwamba walivuta kwa moyo wao wote katika uaminifu, kwa hiyo

haidhuru unavuta kwa uaminifu jinsi gani, huna budi kuwa na Yeye. Kwa hiyo wakavuta, na kuvuta, na matumaini yote yalikuwa yamekwisha, karibu tu kufa.

¹⁶² Na hapo ni karibu mahali lilipo sasa, linaelekea moja kwa moja kuwa la kawaida tena, lile kanisa dogo ambalo wakati mmoja lilikiri utakatifu, likimwishia Mungu, linarudi moja kwa moja ulimwenguni tena, likipenya moja kwa moja. Na kama hawatawaingiza katika *hili*, wanatenda hivi, wataenda kwa lingine, na kutenda namna hiyo. Mnaona? Ukipenya tu kidogo, ibilisi atahakikisha ya kwamba una njia ya kutokea. Hiyo ni kweli.

¹⁶³ Sasa, tunaona ya kwamba haya yote yalikuwa yakitukia, na matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Lakini mnajua nini? Hii hapa sehemu nzuri kuhusu hadithi hiyo: Yeye hakuwa amewaacha. Aliwatuma waende kwenye ufufuo, kupunga mikono, kupeana mikono na watu, na kuwa na yubile. Lakini mnajua alilofanya? Alipanda kilima kirefu zaidi kilichokuwako karibu na pale, kusudi aweze kuwaangalia. Hivyo ndivyo amefanya.

¹⁶⁴ Alipanda Kalvari, wakamkatilia mbali wakamtoa pale, wakamzika, kisha akaanza kupanda, ndipo, “Akapanda mpaka akalipita jua, mwezi, na nyota, Jupita, Zuhura, Neptuni, na Mirihi,” akaendelea tu kusonga mbele, “Akapanda mpaka akaipita nyumba hii ya kale ya udongo, kisha akaenda mbio kwenye ile Njia ya Kilimia Cheupe.”

¹⁶⁵ Alipanda juu sana mpaka akapita Mbingu. Biblia ilisema Yeye huziangalia chini, mwajua. Yeye yuko juu kuliko Mbingu. Jina Lake liko juu ya kila kitu kinachoitwa Mbingu. Alienda kule juu *kabisa*, apate kuangalia nyuma na kuuona ulimwengu mzima. Kama vile ule wimbo wa kale ulivyokuwa ukiimbwa, “Jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia.”

¹⁶⁶ Na moja kwa moja katika saa ambapo matumaini yote ya kwamba ninii. . . Kanisa lilikuwa limejaa maji nalo lilikuwa likielekea upande mbaya, huyu hapa anakuja akitembea moja kwa moja miongoni mwao, nao walimwogopa. Tumaini pekee walilokuwa nalo la kujiokoa na meli hiyo iliyojaa maji katika dhoruba hiyo, waliogopa Tumaini pekee walilokuwa nalo, waliliogopa. Laiti wangaliyajua tu Maandiko! Waliliogopa, nao wakasema, “Ni mzuka, ni roho,” nao wakalia kwa hofu. “Hatuna uhusiano wowote nalo, ni telepathia, ni mpiga ramli.”

Yesu akanena, akasema, “Msiogope, ni Mimi.” Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo, sivyo?

¹⁶⁷ Ninachukia kukomesha ushuhuda huu, lakini ni—ningetaka sisi. . . Ninatumaini sasa, tunapoomba, ya kwamba Yeye atatupa ushuhuda wa kibinafsi. Msiogope, ni Yeye, Yeye yule. Yeye ni Kuhani Mkuu, aliyeketi mkono wa kuume wa Ukuu Wake

Utukufuni, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Na kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa wakati huo, Yeye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako, Naye atatenda kama vile alivyotenda wakati huo, kwa sababu Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁶⁸ Baba Mkuu wa Mbinguni, Yeye aliye na...Hao watu mashuhuri wanaotoa ushuhuda kwetu usiku wa leo, mwandishi, Mathayo, na watakatifu wote wapendwa waliopewa mamlaka ya kuandika Biblia hii. . .

¹⁶⁹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...sema kwamba ni kweli, lakini Mungu, ninaamini ya kwamba hao wanafunzi walipewa mamlaka ya kuliandika Neno, kwa kuwa mwishoni mwa Kitabu, lilisema, “Yeyote atakayeongeza lolote Kwake ama kuondoa lolote Kwake. . .” Ninaliamini, matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu kingine chochote ila Hilo, Bwana, na matumaini ya kundi hili dogo la watu hapa, usiku wa leo. Tunathamini ushuhuda wao unaowekwa na Wewe, kwamba tungeweza kuusoma. Nasi tunasoma Hapo ya kwamba Wewe ni yule yule.

¹⁷⁰ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utaingia, usiku wa leo, miongoni mwa watu. Naye Mungu aliyekuwa katika mwili huo upatikanao na mauti aliyenena na Ibrahimu, Mungu aliyekuwa katika mwili unaopatikana na mauti wa Mwanawe, Kristo Yesu, hebu Mungu yuyo huyo ajitambulisha Mwenyewe, usiku wa leo, katika Kanisa ambalo amelitakasa kwa Damu Yake Mwenyewe, na ameliosha, na kuisafisha hiyo nyumba kutokana na kutokuamini, kisha akaingia akae hata ukamilifu wa dahari kama Yeye alivyoahidi. Kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, ninaomba. Amina.

¹⁷¹ Sasa, naja, si kuwaponya wagonjwa, naja kuwaombea watoto wa Mungu walio wagonjwa. Mimi ku-. . .Mungu huwaponya wagonjwa, na wagonjwa tayari wameponywa, mtu yeyote anajua hilo. Sikuja kuwaokoa waliopotea, nilikuja kuwaambia waliopotea ya kwamba tayari wameokoka, kama tu watalikubali. Nimekuja kuwaambia wale ambao wameokoka, na wanataka ushahidi huu, kwamba wana—wana hakikisho na wameonja karama za Mbinguni kutoka ng’ambo ya Yordani, kule, kama vile Waebrania 6 ilivyosema wangepanya, “wamefanywa washirika wa Roho Mtakatifu na kuonja karama za Mbinguni.”

¹⁷² Kama ungetaka kuionja, ninakupendekezea kwenye Kitabu cha Matendo, ambapo Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Kama hujawahi kubatizwa bado, na umetubu, kutakuwako na ibada ya ubatizo hapa kesho, shuka uje, amini. Unapointia majini, amini ya kwamba Mungu atakupua Roho

Mtakatifu, Atafanya hivyo, ni yale aliyoahidi. Hawezi kusema uongo, hana budi kullitimiza Neno Lake, Naye atafanya hivyo. Wewe njoo ukiamini.

¹⁷³ Na sasa, kama wewe ni mgonjwa usiku wa leo, nakwambia, Yule ninayenena habari zake, wakati alipokufa pale Kalvari, papo hapo, mijeledi mgongoni Mwake, machoni pa Mungu, alinunua uponyaji wako, tayari umeponywa.

¹⁷⁴ Sasa, wana amri za kuwekea mikono. Nafikiri, labda, hivi majuzi tulikuwa na ndugu zetu wa Kipentekoste, kundi lao, kuondoka, afadhali nisiseme hilo. Mimi—mimi si hakimumu wa mtu yeyote, kwa sababu kwamba, mwajua, ninawazia juu ya kuwekea mikono, na kutoa karama, mnaona, karama na miito havina majuto, mnaona, zilikusudiwa kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu kuwa katika mambo hayo, mnaona.

¹⁷⁵ Huenda tukawatambua, na kuwawekea mikono yetu, kama Paulo alivyomfanyia Timotheo pale, kuiidhinisha. Huku wakijua ya kwamba yeye, ile karama ilikuwa ndani yake, waliiona ikifanya kazi, nao wanampa tu mkono wa kuume wa ushirika, kitu kama hicho, kumleta katika utumishi wa Mungu. Na hilo ndilo jambo pekee tunalofanya, kwa kuweka mikono yetu juu ya wagonjwa wanapokuwa wagonjwa, kwa sababu, Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Si kwamba watu hapa... Watu walioamini wangepokea mikono yao juu ya wagonjwa, kama idhini kwamba waliamini.

¹⁷⁶ Sasa, lakini ninaamini ya kwamba Yesu Kristo yupo hapa, ninaamini Yeye yupo hapa katika kila nguvu, na kila kitu alichowahi kuwa duniani, kitu pekee tofauti ni ule Mwili wa kawaida unaoketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Nao uko pale kama sadaka ya amani kwa ajili yako, uko pale kama hakikisho lako ya kwamba kila kitu alichofia, unacho, kama utalikubali na kulliamini. Liamini.

¹⁷⁷ Sasa, ninaamini mwanangu alisema ya kwamba alisambaza kadi za maombi. Kwa kawaida, siku chache za kwanza usiku huko juu, hatukuwa na kadi za maombi, na kwa kawaida hatuwi nazo, bali alisema watu walikuwa wakiomba kadi za maombi, naye akasambaza kadi za maombi. Je, watu hapa ndani wana kadi za maombi? Hebu tuone. Ye—yeye huzichanganya pamoja, na kumpa mtu yeyote kadi za maombi anayezitaka.

¹⁷⁸ Mtu yeyote ambaye amekuwa kwenye mikutano hapo awali, anajua ya kwamba kuna wengi zaidi wanaoponywa kwenye mkusanyiko kuliko walio jukwaani. Si lazima uwe na kadi za maombi, ni kumleta tu mtu hapa juu kuwaombea, hivyo tu. Sasa, nitakuja kuomba, ninyi aminini.

¹⁷⁹ Sasa, Billy yuko wapi? Je, aliingia? Alisambaza kadi zipi za maombi? Sijui. Ilikuwa ni ipi? Kuna yeyote aliye na kadi za maombi moja? Hebu tuone kama kuna mtu kama huyo hapa. Kadi za maombi namba moja. Kuna mtu aliye nayo? Inua mkono

wako. Kadi ya maombi namba moja. Vema, labda kamwe... Labda alianza mahali pengine basi. Kadi ya maombi namba moja. Hakuna mtu aliye na kadi ya maombi moja? Mbili. Ni nani aliye na kadi ya maombi mbili? Vema, basi alianza hapo basi. Vema, Bwana.

¹⁸⁰ Kadi ya maombi moja, mbili, tatu, simama. Sasa, huenda... Angalia kote kwenye kadi ya mtu fulani, huenda ikawa ni kiziwi na hawezi kusikia, mnaona. Wana kadi ya maombi moja, mbili, na tatu. Sasa, ninamwona mtu mmoja tu amesimama. Moja, mbili, tatu. Ninamwona huyu. Yako ni ipi? Tatu. Hapa kuna mbili. Namba moja iko wapi? Vema, kama hawaingii... Wasemaje? Vema. Njoo. Naam, Bwana. Naam. Hilo ni sawa. Vema, Bwana.

¹⁸¹ Namba moja, mbili, tatu. Sasa, njoni huku, tafadhali, ninyi nyote mlio na kadi za maombi njoni papa hapa, moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, simameni. Nne, tano, sita, vema, chukua mahali pako papa hapa. Saba, nane, tisa, tisa. Loo, sawa. Saba, nane, tisa. Sidhani tutakuwa na nafasi kubwa mno hapo, kusimamisha wengi kupita kiasi. Saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja. Huko nyuma kabisa. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na tatu. Kadi ya maombi namba kumi na tatu.

¹⁸² Sitaki kumkosa mtu yeyote, maana tunataka kumwombea kila mtu aliye na kadi ya maombi, mnaona, nao wanakuja na kuchukua kadi ya maombi. Lakini usichukue—usichukue kadi yako, unaondoka, wala hurudi, unaona, mtu fulani anapaswa kuipata.

¹⁸³ Kadi ya maombi kumi na tatu. Tutangojea kidogo tu, labda ni mama aliye na mtoto mchanga, ama chochote kile, ama ilimbidi atoke nje, ama chochote kile, huenda akarudi katika dakika moja.

¹⁸⁴ Tutaanzia papa hapa basi, na tuanzia kwenye idadi hii, na kuwaombea, mpaka sisi... Ni wangapi ambao mmewakosa? Wote hapo, hadi kumi na tatu? Wasemaje? Namba kumi na tatu haipo. Vema, tutakomea papo hapo sasa, mpaka watakapoingia.

Vema, Bwana. Hebu... Ndugu Bigby, kama utaninii... Sasa, pokea kadi zao za maombi kule chini, Ndugu Bigby, tafadhali. Vema.

Sasa, njoo huku, Bwana. Simama tu papo hapo, kwa muda kidogo tu.

¹⁸⁵ Sasa, ninaamini mtu huyo ni mgeni kwangu. Sisi, hatufahamiani, lakini, nijuavyo mimi. Yeye ni mgeni kwangu. Nasi hatufahamiani, lakini Bwana anatumia sote wawili, sivyo? Naam.

¹⁸⁶ Basi ni wangapi huko nje, ambao hawana kadi za maombi, na hata hivyo unaamini Yesu atawaponya, unataka Yeye akuponye? Inueni mikono yenu. Ni wengi kweli. Sasa, sio

lazima uwe na kadi ya maombi. Nitasema hivi: Fanya kama yule mwanamke alivyofanya kwenye... aliyetokwa na damu. Mnajua, hakuwa na, tungeita, tuseme, kadi ya maombi, bali alijipenyeza tu mpaka akaligusa vazi Lake. Mnakumbuka hilo? Ndipo ikamsimamisha.

¹⁸⁷ Sasa, Yeye hakuhihi hilo kimwili, kwa sababu vazi la Kipalestina linapwaya. Na kila mtu pamoja na ninii yao... Mbona, hata Petro alimkemea, kasema, "Bwana, kwa nini useme jambo kama hilo? Mbona, kila mtu anakugusa Wewe."

¹⁸⁸ Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu." King James inasema, "nguvu zimeondoka," ambapo, *nguvu* ni "uweza." Na, "Nimekuwa dhaifu," ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akampata mwanamke ambaye amegusa vazi Lake, Naye akamwambia ya kwamba imani yake ilikuwa imemwoko, kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁹ Sasa, sikilizeni kwa muda kidogo tu sasa, itawafaa sana. Sasa, je, Maandiko yanasema ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele? Nadhani *hawa* ni wahudumu. Sasa, je, Maandiko yanasema, katika Kitabu cha Waebrania, ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa? Yeye anaishi daima kufanya upatanisho, mnaona, Naye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Vema, basi kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, na kama unaweza kungusa Yeye...

¹⁹⁰ Unasema, "Ndugu Branham, nitatembea na kungusa Ndugu Bigby." Vema, hilo lingekuwa ni jambo zuri kuonyesha ushirika wako, ama upendo wako kwa Ndugu Bigby. "Ndugu Branham, nitakuja nikuguse." Vema, hilo lingekuwa zuri, bali hakuna nguvu ndani yetu, sisi ni wanadamu, yeyote wa hawa wahudumu hapa, sisi ni wanadamu, kwa hiyo isingefaa chochote kuja hapa. Lakini kwa nini usikumbuke tu kwamba umefufuka pamoja Naye? Nawe umeketi pamoja Naye, baraza la Mungu, Kristo, umeketi pamoja na Kristo sasa, mamlaka yote yako papa hapa pamoja nawe. Kwa hiyo kwa nini usiguse tu vazi Lake kwa imani?

¹⁹¹ "Bwana, nina haja, mimi ni mgonjwa, na, Baba Mungu, jalia nikuguse Wewe usiku wa leo, ninakuamini Wewe. Naye Ndugu Branham amekuwa akitusimulia mchezo mdogo wa kuigiza, lakini ulikuwa ni kweli, huo mchezo wa kuigiza ulikuwa naye akatupa Maandiko machache pale yanayoonyesha ya kwamba Wewe ni yeye yule, Nawe huna budi kuwa yeye yule. Kwa hiyo anasema ya kwamba Wewe uko hapa katika umbo la Roho kufanya kazi leo hii, kama ulivyoahidi kabla ya kule kuja tena, ya kwamba ungekuwa *hivyo*..."

¹⁹² Mnajua, kuna tofauti kati ya *kuonekana* kwa Kristo na *Kuja* kwa Kristo, hayo ni maneno mawili tofauti kabisa. Yeye

anaonekana sasa katika Kanisa Lake, tunamwona, tunajua ni Yeye. Ni Roho Mtakatifu, mnaona, tunajua Ndiye.

¹⁹³ Sasa, tunaamini ya kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu, sisi sote tunajua hilo. Ba...kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, hatuamini kuna Miungu watatu, tunaamini kuna ofisi tatu za Mungu yeye yule. Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu ni ofisi tatu ambazo Mungu yeye yule amefanya kazi ndani yake. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Mkabatize, mkitumia Jina,” cheo, “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” mnaona, ambapo hawasemi, “Miungu watatu,” bali wanamaanisha, “Mungu mmoja katika ofisi tatu,” Mungu yeye yule, Miungu watatu ingekuwa ni ukafiri, mnaona, lakini ni—ni Mungu mmoja, Yuko katika ofisi tatu.

¹⁹⁴ Ubaba, si hata m—mnyama angeweza kuugusa ule mlima, hana budi kupigwa mawe, ama kuchomwa m—mkuki. Hiyo Nguzo kuu ya Moto, kisha hiyo Nguzo ya Moto ilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Ni kitu gani? Mungu, akijidhili; tulimhisi Mungu, tukamgusa Mungu, Mungu alidhihirishwa katika mwili miongoni mwetu. Yesu alisema, “Si Mimi nikitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu, Yeye anaishi ndani Yangu.”

¹⁹⁵ Ndipo akasema, “Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.” Ndipo Ye—Yeye akafa, akasulubiwa, akafufuka siku ya tatu, na baada ya kupaa Kwake, Paulo alikuwa akienda zake Dameski, siku moja, kuwakamata Wakristo fulani, ndipo Nguzo iyo hiyo ya Moto ikaanguka mbele zake, hata ikayapofusha macho yake. Hao wengine hawakuiona, lakini ilikuwa halisi sana kwake ikampofusha. Naye akasema, “Bwana, u Nani Wewe?”

Naye akasema, “Mimi ni Yesu.”

¹⁹⁶ Na kama Mungu yeye yule, Roho Mtakatifu, akitenda kazi miongoni mwetu, basi anajidhihirisha Mwenyewe katika miili yetu, kama alivyofanya wakati huo. “Kwa hiyo ninaamini jambo hilo, Mungu. Sasa, ninazungumza nanyi kama mwaminio. Sasa, Wewe nena jinsi ulivyofanya kupitia Kanisa Lako.” Mbona, huyo ni Yeye Ambaye, unaponena kwa lugha zisizojulikana, nao wanaifasiri, na kusema kweli, Huyo ni Mungu, Huyo ni Mungu ndani yenu. Mnaona?

¹⁹⁷ Mnaona, yote aliyokuwa Mungu Yeye aliyamimina ndani ya Kristo, yote aliyokuwa Kristo aliyamimina ndani ya Kanisa, kwa hiyo ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, mnaona. Mnaona? Sasa, ninyi aminini tu, na mwangalie *huku*, na kusema, “Bwana Yesu, ninaamini,” naye Mungu atamshusha Roho Wake, na tuone kama Yeye hafanyi vile vile alivyofanya huko nyuma.

198 Sasa, iweni tu na kicho. Msininii tu. . . Nawatakeni mumsifu Mungu, lakini mnapoyakaribia mambo haya, njoni kwa kicho kabisa.

199 Sasa, huyu hapa mtu, na hii hapa Biblia yangu, sijawahi kamwe maishani mwangu kumwona mtu huyu nijuavyo mimi. Huenda alikuwa mkutanoni mahali fulani, na labda hajawahi kuniona. Kama imekuwa, imekuwa mahali fulani ambapo amekuwa mkutanoni, ama mahali fulani, na labda anione, ama. . . Umewahi kuniangalia hapo awali? Hujapata kuniona maishani mwako. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana.

200 Sasa, kama. . . Mtu huyo, huenda ni mgonjwa, huenda amesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine, huenda ana matatizo ya kinyumbani, huenda akawa na matatizo ya kifedha, huenda akawa ni mdanganyifu. Na kama ndivyo alivyo, angalieni kitakachotukia. Mnaona? Angalieni tu, mnaona. Sijui mimi. Lakini kama Roho Mtakatifu anaweza kuja hapa, na kuwaambia wageni wawili, amwambie jambo ambalo limekuwa, ama jambo fulani kumhusu, ama kilichomleta hapa, naye atajua kama ni kweli ama si kweli, ata—atathibitisha hilo. Halafu basi, kama Yeye anaweza kumwambia kile kilichokuwako, hakika angeamini, kama ungemwambia kile kingekuwa. Bila shaka. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu tuna imani katika Biblia. Mnaona? Mnaona? Ni kweli.

201 Nami nashangaa ni wangapi wenu wasafiri, usiku wa leo, wageni hapa mjini, na vitongojini, wangeamini, na kujua ya kwamba isingewezekana kwangu, mwanadamu, kufanya hivyo? Mbona, hakika, ingekuwa, kama wewe ni mzima kiakili, ungeliamini. Unaona? Haiwezekani kabisa. Kwa hiyo ingebidi kuwe na namna fulani ya nguvu kufanya hivyo, unajua angefanya hivyo. Vema, sasa, inategemea unafikiri ni nguvu gani, thawabu yako itatoka wapi. Unaona?

202 Sasa, Mafarisayo walisema, walipoiona, “Ni Beelzebuli,” bali waaminio walisema, “Ni Mwana wa Mungu.” Sasa, tunajua Maandiko yameahidi jambo hilo katika siku hii ya mwisho, sivyo? Yeye aliahidi jambo hilo, tunajua.

203 Wasikilizeni hawa wahudumu hapa wakisema, “Amina.” Mnaona? Hao ni wachungaji wenu, wanajua wanalozungumzia. Mnaona? Wanajua jambo hilo. Nami ni ndugu yao, raia mwenzao wa Ufalme, nikifanya kazi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Wao ni makasisi, wasemaji, wahubiri mashuhuri wenye nguvu, mimi si ninii, hii ni huduma yangu, huu ni wakati ninapohubiri, kwa karama tu. Nami ninawapenda watu sana, naye Bwana alinjalia kuwahubiria namna hii.

204 Sasa, kama Roho Mtakatifu atasema mambo haya, na kufanya hivyo, je, itawashawishi, kila mmoja, ya kwamba Yesu Kristo yu hai leo, na Yeye yuko hapa tena? Ingekushawishi, sivyo, Bwana? Hakika ilimshawishi Nathanaeli, yeye alikuwa

ni mwaminio, kwa sababu haidhuru yeyote wa hao wengine alisema nini, hakika ilitenda kazi kwake, naye alijua.

205 Haikuleta tofauti yoyote kama watu huko Sikari walimwamini mwanamke huyo au la, alikuwa na ujuzi, alijua, Yeye alimwambia shida yake ilikuwa ni nini.

206 Anajua shida yako, ni koo lako. Hiyo ni kweli. Hii inaweza kukusaidia: Unahitaji koo hilo, kwa sababu wewe ni mhubiri. Itakuwa sawa. Endelea. Itakuwa sawa.

Bila shaka Mungu anawapenda watu Wake.

207 U hali gani, Dada? Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Amina. Hii hapa picha tena, ambayo nilikuwa nikizungumzia, hao hapo mwanamume na mwanamke wamekutana kwa mara ya kwanza, nadhani. Hatufahamiani. Kwa hiyo kama watu huko nyuma huenda wasiweze kukuona ukitikisa kichwa chako, waweza kuinua tu mkono wako, niliposema, “Hatufahamiani”? Sikujui, wala wewe hunijui.

208 Sasa, hii hapa picha kama ya kile kisima huko Samaria, ambapo Bwana wetu alikuwa ameketi, na mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara yao ya kwanza maishani. Simjui, yeye hanijui. Yeye ni mwanamke tu, alishuka chini muda mfupi uliopita. Na—na huenda aliinua mkono wake, naye mvulana akampa kadi ya maombi, na, hapa, na, imetokea kwamba amesimama hapa mstarini, hakuna lingine.

209 Sasa, yafuatayo hayana budi kuwa ni Mungu. Lakini kama Yeye ni Mungu yeye yule, Naye yuko ndani yako, Naye yuko ndani yangu, nayo maisha yetu yamewekwa wakfu Kwake, Naye ametoa karama ambayo mimi hujisalimisha tu Kwake, na halafu Yeye ananionyesha ono, kisha nitasema, wakati tu ono likiendelea, kile kilichotukia, nawe utajua kama ni kweli ama si kweli. Nafikiri huyo mwingine ambaye ndiyo kwanza apite alikuwa ni mwanamume, huyu ni mwanamke. Mnaona? Ndipo utajua.

210 Jambo la kwanza, huyu mama anaugua ugonjwa mbaya wa mishipa, ana wasiwasi sana. Ana, kwa namna fulani, matatizo, mambo mengi yanayomsumbua. Sasa, hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, ili watu waone.

211 Ninashika roho yuyo huyo sikuzote, akisema, “Alibahatisha.” Sibahatishi hilo, enyi marafiki, huko si kubahatisha. Sasa, ninyi kumbukeni, ninashika mawazo yenu. Mnaona? Mnaona? Nilikuwa nikiwataja hadharani, wengi wenu mnajua jambo hilo, ndipo linaumiza hisia. Um-hum. Mnaona? Ni wangapi wamekuwa mikutanoni, na kumwona mwanamke na wanaume, wakimvuta mwanamume moja kwa moja kutoka mkutanoni, na huyu *hapa*, na kuthibitisha walikuwa wakiishi katika uzinzi? Mneona hayo yote, na kila kitu kilichotukia. Mnaona? Lakini inakubidi kuangalia. Nina hekima zaidi kidogo

tangu wakati huo, mnaona, maana Yesu alisema acheni ngano na kadhalika zikue pamoja, mnaona.

Huyu ni mwanamke mzuri, ana hisia nzuri kwa roho yake. Wakati akiwa na hiyo, hebu tuone kama nilikuwa nikibahatisha.

²¹² Nilisahau. Alisema, loo, naam, ninauona sasa: “wasiwasi, fadhaa, kusumbuliwa.” Naam, unasumbuliwa na jambo baya sana, unaogopa kansa. Hiyo ni kweli. Na hiyo kansa iko, si katikati, iko kwenye titi lako la kushoto, hiyo ni kweli. Unaogopa hiyo, sivyo?

²¹³ Unamhofia mtu mwingine pia. Unataka nikwambie? Ni sawa? Ni binti yako. Unataka nikwambie ana shida gani? Ana u—ugonjwa wa damu. Amekuwa hivyo kwa muda mrefu, kutokwa na damu. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa? Unaamini wewe, utakaporudi, utamkuta mzima? Nenda ukiamini. Usininii. . . Amini. . .? . . . Hiyo ni kweli. . .? . . .

²¹⁴ Amina. Mnaona? Ana ushuhuda. Sasa, huyabahatishi mambo hayo, rafiki. Usiwe tu na shaka sasa, usiwe na shaka.

²¹⁵ Kabla sijaanza mstari wa maombi, mwajua, kuwaombea watu. . . Nafikiri hao ni kama wawili, watatu ni shahidi, ama, thibitisho; nafikiri hiyo ni kweli, sivyo?

²¹⁶ Mama mzuri aliyesimama hapa, hatufahamiani, nadhani. [Dada huyo anasema, “Loo, la, nilikuwa kwenye mstari wako wa maombi, ulipokuwa hapa hapo awali.”—Mh.] Loo, ulikuwa kwenye, vema, kwenye mstari wa maombi nilipokuwa hapa hapo awali. Vema, bila shaka, nisingejua hilo, mwajua, maelfu mengi sana. Sina hata fununu wewe ni nani, ama kilichokuleta hapa, ama chochote kama hicho. Hiyo ni kweli. Nisingejua, bali Yeye anajua.

²¹⁷ Kama atanifunulia, je, utakubali uponyaji wako basi? Vema, kama utaamini kwa moyo wako wote, una wasiwasi pia, na matatizo, na kufadhaika, bali kamwe haitakubidi kufanyiwa upasuaji huo wa uvimbe huo ubavuni mwako, utakuacha, kama utaamini. Utaamini? Nenda zako, useme, “Asante, Bwana Yesu.” Amini kwa moyo wako wote. [Dada huyo anauliza, “Ngoja, sasa hivi haitanilazimu kufanyiwa upasuaji?”—Mh.] Amini tu kwa moyo wako wote, haitakubidi kufanyiwa, la, iwapo tu utaamini. Unaona, hiyo ni imani yako sasa. Unaona? Mimi. . . Amini tu, usiwe na shaka.

U hali gani, Mama? Hatufahamiani?

²¹⁸ Hebu kidogo. Huyu ni mwanamke tofauti. Sasa, iweni tu na kicho na muombe. Kumbukeni tu, una, unaweza tu kuwa na mawazo mawili niani mwako. Nami ninashukuru mko sahihi asilimia tisini na tisa, mnaona, mnaamini ni Mungu, na ni Mungu. Hebu kidogo. Wazia tu Bwana wetu, Yule ambaye tutampenda, na kumlaki, na kupaa juu kumlaki, sisi ni (Mwajua, alitoka wakati wa jioni kutembea kondeni, naye yule mrembo

Rebeka hakuwa amemwona kamwe, alikuwa tu amesikia habari zake. Akaruka kutoka kwenye ngamia, na kukimbia kumlaki.), Yeye tayari, labda, ameondoka Utukufuni akishuka, tuko njiani mwetu kumlaki sasa, tukipitia moja kwa moja kwenda nchi ya Kanaani.

Jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko, mwanamke mwingine alitokea hapa, si mwanamke huyu.

²¹⁹ Naam, ninamwona sasa, ameketi kule nyuma akiomba. Usiogope, utakuwa mzima. Miguu yako inakusumbua, kwa sababu ulikuwa katika ajali ya motokaa. Umevaa nguo ya kijani kibichi, na ilikuwa ya kijani kibichi tofauti na hii, kwa hiyo haya basi. Usijali, utapona.

²²⁰ Simjui huyu mama, hatufahamiani. Roho, ile Nuru inayoning'inia karibu na huyo mama, ilionekana kuvuka hadi kwa mama huyo mwingine anayeketi karibu naye. La, si huyo mama, yeye anamwomba mtoto, ni msichana mdogo aliye na ugonjwa wa tumbo, ambaye yuko tayari kufanyiwa upasuaji. Huo ni mkono wake ulioinuliwa, uweke juu ya huyo mtoto, hapo.

²²¹ Baba wa Mbinguni, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu, zilizoko sasa, anayejua siri za moyo... Bwana, wanajua nisingeweza kuponya, kwa sababu tayari umefanya hivyo, lakini Uwepo Wako unawafanya waamini, Bwana. Na kama mwanamke yule alikuwa na imani ya kutosha aliyegusa vazi Lako kukuvuta ndani mle, hakika mtoto huyo mchanga atakuwa sawa. Ninalitamka hivi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Iweni tu na imani.

²²² Mtu yule aliyeketi upande mwingine, karibu sawasawa na mahali walipo, ambaye ana ugonjwa huo wa mgongo, aliyeketi hapo: Bwana, kama utaamini kwa moyo wako wote (Kwa namna fulani analia, akiangalia.), kama utaamini, ugonjwa wako wa mgongo utakuacha, utakuwa sawa. Mungu awabariki. Yote yamekwisha sasa, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima.

Unafikiri nini? Yeye si ni wa ajabu? A-ha, hakika ndivyo alivyo.

²²³ Hatufahamiani. Hilo hapo tena, si—si hili, loo, ni, unasimama kwa ajili ya mtu aliye na ugonjwa wa mguu, ni dada yako, hivyo ndivyo ilivyo. Naam. Hiyo ni kweli. Niliona miguu, na watu ambao... Naam, unamtaka aje kanisani, umlete, ha—hata asingeweza kuvaa viatu vyake na kadhalika. Unaamini? Wewe rudi, na umkute jinsi ambavyo wewe... .

²²⁴ Unaamini Roho Mtakatifu asiyekosea, Mungu, Baba yetu? Yeye ni mtukufu, wa ajabu, Bwana wetu. Lakini sisi, hatuna budi kumwamini Yeye kwa moyo wetu wote, hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kupata baraka zetu kutoka Kwake, ni kumkubali, kumwamini.

225 U hali gani? Nadhani hatufahamiani, Mungu anatumia sote wawili. Je, unaamini ya kwamba hisia hiyo uliyo nayo sasa . . . ? Sasa, kusingekuwako na hisia kama *hiyo* kutoka kwangu. Mnaona, si—siwezi kuelezea jambo hili, ni kama kiwango kingine, lakini moja kwa moja karibu nawe sasa, kuna Nuru, ile ambayo ninyi nyote mnayo hapa kwenye picha. Hiyo ndiyo inayomfanya ajisikie hivyo, kusimama karibu na mwanadamu kusingefanya hivyo. Mnaona? Sasa, inasonga kati yangu na wewe.

226 Naam. Uko hapa, nawe ni mgonjwa sana, una ugonjwa wa figo unaokusumbua. Na shida yake ni kwamba, kwamba mafigo yako ya—yameshindwa kufanya kazi, kutupilia mbali hiyo sumu, nayo inalundikana na kukusumbua. Hiyo ni kweli. Unaamini? Hutoki hapa, unatoka Charleston. Unaamini kwa moyo wako wote? Yeye si ni wa ajabu? Sikiliza, Pearl, nenda zako.

Unaamini?

227 Yeye huponya pumu pia, unaamini hilo, sivyo, Dada? Amina. Nenda ukiamini kwa moyo wako wote, nawe unaweza kupata kile unachoomba. Amina. Mungu akubariki.

Kisukari si kitu kwa Mungu kuponya. Yeye ni Mponyaji halisi, sivyo? Amina. “Kama unaweza kuamini.”

Yabisi kavu huwalemaza wengi, bali kama utaamini, haitakulemaza, amina, kama utaamini tu.

Iweni tu na imani. Je, mnaamini?

228 Hukupata kusikia yale yaliyoambiwa huyo mwanamke mwingine, ila yabisi kavu. Anaweza kukuponya pia. Unaamini hilo? Vema, endelea tu moja kwa moja, ukisema, “Bwana Yesu ashukuriwe.” Amina.

Sasa, Ndugu, unaamini? Nenda ukale chakula chako cha jioni basi. Kula kitu fulani, maskini kidonda hicho kitakuacha na unaweza kwenda nyumbani, uponywe.

229 Unaamini? Ugonjwa wa mgongo, figo. Unaamini utakuacha? Basi nenda zako, na uanze tu kushangilia, na kusema, basi, “Mungu na ashukuriwe,” kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote, bali huna budi kuamini.

230 Hebu kidogo. Kitu fulani mahali fulani. Mwanamume mdogo kuliko huyu, hapana shaka alikuwa kwenye kusanyiko. Hapa, ngoja. Naam, wewe uliyeruka wakati uo huo, kigugumizi. Mungu anaweza kuponya tatizo la kigugumizi, kama utaamini, ikiwa tu utakuwa na imani.

231 Wewe huko uliyeinua mkono wako, huyo mama hapo mwishoni uliye na kansa kwenye titi lako la kushoto, inua mkono wako. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya na kukuponya?

Vema, Bwana. Unaamini Yeye alikuponya wakati uo huo? Nenda zako, na ufurahi, na kushangilia, ukisema, “Asante.”

²³² Na tuendeleo na ushuhuda wetu. Yeye si ni wa ajabu? Je, anaweza kusema uongo? La hashu. “Msiogope, ni Mimi.” Kwa nini usimwalike Yeye kwenye hiyo mashua ndogo usiku wa leo? Je, wewe ni mgonjwa? Inueni mikono yenu, enyi watoto. Inua mkono wako, enyi waaminio. Sasa, weka tu mikono yako juu ya mtu fulani aliye karibu nawe, ulisema ulikuwa mwaminio.

²³³ Sasa, Yule, ambaye ni Mungu wetu na Mfalme wetu, Yule aliye hapa pamoja nasi usiku wa leo, ametupa hakikisho ya kwamba wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya. Mnaamini hilo? Mnaogopa? Mnaogopa? Au mnampenda? Mnaamini ni Yeye? Basi mkaribishe ndani, useme, “Ingia ndani yangu, Bwana Yesu. Ingia moyoni mwangu, usiku wa leo, Na—nataka unipitishe salama katika safari hii, nami nitakuwa mzima.”

²³⁴ Sasa, wewe mwombe mtu uliyemwekea mikono. Usijiombe sasa, wewe omba tu kwa ajili ya . . . Mtu huyo anakuombea, wewe omba tu . . . Nitamalizia kadi kesho usiku. Weka mikono yako . . . Ama huenda isikubidi kuwa na yoyote kesho usiku. Wekeaneni tu mikono, nanyi mtaenda nyumbani, mpate afya.

²³⁵ Baba yetu wa Mbinguni, tunaleta kwenye kusanyiko hili, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Shetani amepulizia pumzi yake, amejaribu kuwaambia watu . . . Mara nyingi, watu wamewapeleka kwenye barabara mbaya. Lakini, usiku wa leo, sisi, tuna hakika ya kwamba huu ni Uwepo Wako, na Wewe unawaambia, “Msiogope, ni Mimi, msiogope.”

²³⁶ Ninaweka mikono yangu juu ya lesi hizi zilizowekwa hapa, ni wagonjwa na wanaoteseka. Ee Mungu, jalia nguvu za Mungu zimkemeo kila ibilisi ambaye amewafunga watu hawa, na katikati ya watu.


²³⁷ Na Shetani, ewe asiyeamini, huwezi kuwashikilia watu hawa, huwezi kuwafanya wasiamini tena. Wanajua kwamba Mwana wa Mungu amefufuka katika wafu kwa muda wa miaka elfu mbili, na kwamba Uwepo Wake upo hapa sasa, katika umbo la Roho Mtakatifu. Huwezi kuwadumisha wagonjwa tena, huwezi kuwadumisha namna hii. Toka ndani yao, katika Jina la Bwana Yesu, toka ndani ya kila mmoja wao wapate kuponywa.

²³⁸ Wamewekeana mikono, wao ni waaminio, Yesu, Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.” Ni ahadi Yako, Bwana.

Toka, Shetani, na uwaache watu hawa wawe huru.

²³⁹ Wote wanaoamini, na kukubali uponyaji wenu kutoka kwa Kristo, tupa tu chini kadi yako ya maombi, na usimame kwa miguu yako, na useme, “Siogopi, Bwana, ni Wewe, nami

ninakukubali.” Kama utafanya hivyo kwa imani, utapokea uponyaji wako, kama unaweza kuamini. Liamini tu.

Unaamini hilo? Basi simameni kwa miguu yenu na mkubali uponyaji wenu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Ninakupa...?... 

62-0611 Ni Mimi, Msiogope
Central Assembly Of God
Columbia, South Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org